# Kwa Nini Ilipaswa Kuwa Ni Wachungaji
Tucson, Arizona, USA
Desemba 21, 1964

1 … Nadhani, kwa namna fulani ni mhubiri wa maneno mengi ya kuchosha. Na bila elimu, na—nafikiri sijisikii kama mhubiri kwa watu fulani. Na—na hata sidai kuwa mhubiri, kwa namna fulani mimi ni tairi ya spea. Lakini ninajisikia ya kwamba nina Ujumbe kutoka kwa Mungu, kwamba kwa njia yangu (ya kwamba njia pekee ninayopaswa kuielezea), ninajaribu kuielezea kwa ulimwengu. Na kama sikudumu na Ujumbe huo, ningekuwa msaliti kwa Mungu na mnafiki kwako. Mtu ambaye atasema jambo moja na kuamini lingine, ni unafiki. Inatupasa daima kusema kweli kutoka moyoni mwetu. Ili kwamba wakati watu wanapotutazama, hata ingawa hawakubaliani nasi, tunataka kuwa wanaume na wanawake wenye heshima: kwamba tuseme kutoka moyoni mwetu, yale yaliyo ya kweli mioyoni mwetu.

2 Mwaka jana, ama mwaka mmoja kabla ya mwaka uliopita, nilikuwa na majaliwa ya kuhubiri M—Mkristo…ama samahani, ujumbe wa Krismasi, hapa Ramada. Nami naamini nilizungumza juu ya somo hili, ama hapa ama Phoenix, juu ya: Kwa nini Bethlehemu Mdogo? Nami naamini basi ilikuwa hapa, mwaka jana, nilizungumza juu ya: Tumeiona Nyota Yake Mashariki Na Tumekuja Kumwabudu.

Na, unajua, tunasoma Biblia, nasi tunashangaa, hizo "Kwa nini?" Na usiku wa leo niliwazia, kama mngevumilia kidogo, na kuomba pamoja nami, ningejaribu kuwapa ujumbe wangu wa Krismasi. Mungu anajua tu mahali tutakapokuwa Krismasi ijayo, kama kuna Krismasi ijayo baada ya hii. Kwa hiyo kwa kuwa huenda ikawa hii ndiyo Krismasi ya mwisho tuliyoketi pamoja, mpaka tutakapoketi kwenye meza nyingine. Na haitakuwa ni ya aina hii, bali itakuwa wakati tutakapokula na kunywa ushirika upya pamoja Naye, katika Ufalme wa Baba mwishoni mwa safari. Halafu basi, hebu na tuukaribie usiku wa leo kana kwamba huu ulikuwa ndio ujumbe wa mwisho wa Krismasi ambao tungeketi pamoja, katika kina cha uaminifu.

3 Ninataka kuzungumza usiku wa leo juu ya somo lisilo la kawaida, lakini wakati mwingine unamwona Mungu katika jambo lisilo la kawaida. Yeye hufanya mambo kwa njia isiyo ya kawaida. Si njia ya kawaida, ni njia isiyo ya kawaida, nyakati zisizo za kawaida, matukio yasiyo ya kawaida, Yeye si wa kawaida. Nami ninataka hii … Bwana akipenda, ninataka kuzungumza juu ya somo la: Kwa Nini Ilibidi Iwe Ni Mchungaji.

Na sasa kabla tu hatujaliendea Neno, ambalo naamini hilo ni Mungu, "Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili akakaa kwetu."

4 Kama nilivyosema, juma lililopita, ama juma lililopita huko Phoenix, "Imethibitishwa ya kwamba kuna raia wa dunia hii, watu, wanaopita kwenye jengo hili sasa." Televisheni inathibitisha jambo hilo. Iko katika kiwango kingine, macho yetu ya kawaida na hisi zetu tano haziwezi kuchukua hilo. Si kwamba televisheni hutengeneza cho chote, inazipitisha tu. Huwezi kupiga hatua kwa kidole chako, huwezi kupepesa jicho lako, bali imethibitishwa kuwa imerekodiwa milele. Huenda nimesimama … Ama mtu huko Australia, angekuwa na skrini ya te—televisheni hapa, si hilo tu bali m—mtu huyo angeweza kuzungumza, kusogeza kidole chake, kupepesa jicho lake, ama hata rangi ya nguo anazovaa, zingeonyeshwa hapa ukutani; naye akiwa Afrika, Australia, kote ulimwenguni. Mnaona, kuna duara ya mawimbi ya anga za juu. Siwezi kulielezea, bali ninajua liko. Sidhani mtu ye yote angeweza kulielezea. Kwa hiyo, televisheni inaweza kuingiza hili ndani na kulifanya halisi kwa vyombo fulani, ili waweze kuakisi kwenye ukuta.

5 Sasa, jambo lile lile lilikuwa hapa wakati Adamu alipokuwa hapa. Televisheni ilikuwa hapa wakati—wakati Eliya alipoketi juu ya Mlima Karmeli. Ilikuwa hapa wakati Martin Luther, yule kasisi kijana, alipotupa ushirika sakafuni na kusema, "Ni mkate mwembamba! Na wenye haki wataishi kwa imani." Ilikuwa hapa wakati huo, lakini sasa tunaipata. Na pia ni hivyo, kwamba mbele zetu usiku wa leo ni Mungu, Malaika, viumbe vya kimbinguni ambavyo havionekani kwa macho yetu ya kawaida ya kuona. Lakini siku moja itakuwa halisi kama tu televisheni ilivyo sasa, na ni ya kawaida tu. Sasa, hiyo ndiyo sababu ninaamini Neno.

Yesu alisema, "Ye yote atakayeongeza neno moja kwenye Biblia hii, ama kuondoa Neno moja kutoka Kwake, sehemu yake itaondolewa katika Kitabu cha Uzima."

6 Kwa hiyo, hebu na tuinamishe vichwa vyetu basi, kabla hata hatujalisoma. Kwa makini sana! Mtu ye yote aliye na nguvu za kimwili angeweza kufungua ukurasa, bali ni Mungu tu anayeweza kulifunua.

Na huku vichwa vyetu vimeinamishwa sasa kuelekea mavumbini tulikotoka, na siku moja tutarudi, nashangaa … Na katika wakati huu wa uchaji, tunapokaribia Krismasi, kama kuna wengine hapa ambao kweli wanajisikia wasiostahili na wangependa kukumbukwa katika maombi haya, je, (bila kuinua kichwa chako) ungemwinulia Mungu mikono na kusema, "Nikumbuke, Bwana, Krismasi hii"? Mungu akubariki.

7 Baba wa Mbinguni aliye Mtakatifu sana na Mwenye Neema, Mwenyezi Mungu, Yeye aliyekuwako tangu mwanzo, kabla hakujakuwako na nyota, ama atomi, ama molekuli. Ulifanya vitu vyote katika Yesu Kristo Mwana Wako, nawe umetupa vitu vyote bure katika Yeye. Tunakushukuru, usiku wa leo, Bwana, kwa nafasi hii ambayo umetupa kukusanyika pamoja, kuonywa na kufundishwa na Roho Mtakatifu. Naye Roho Mtakatifu huyachukua maneno Yako na kutufunulia sisi, kwa kuwa Yesu alisema, "Yeye atakapokuja Roho wa Kweli, Yeye atawakumbusha mambo haya niliyosema na pia kuwaonyesha mambo yajayo."

Mungu, hakuna hata mmoja miongoni mwetu, wala hakuna mtu duniani, anayestahili kujaribu kufasiri Neno Lako, kwa maana imeandikwa ya kwamba, "Neno la Mungu si la kufasiriwa na mtu binafsi." Kwa hiyo, Bwana, tunaomba ya kwamba Roho Mtakatifu atatupa usiku wa leo, kila mmoja, kila sehemu tunayohitaji kutosheleza njaa hiyo iliyo mioyoni mwetu kwa ajili ya kutembea karibu na Wewe. Sisi hatufai, ni wachafu, hatustahili. Jalia Mtoto aliyezaliwa Bethlehemu, aliyeishi maisha makamilifu sana, na alikuwa mtu pekee mkamilifu duniani, na akajitolea Mwenyewe fidia apate kutusafisha sisi wenye dhambi na kutufanya tuwe katika uhusiano na Baba, tujalie usiku wa leo. ya kwamba Roho Wake Mtakatifu (kwa kuhubiriwa kwa Neno) atatufanyia jambo hilo.

8 Bwana Mungu, kuna wengi walio wagonjwa nchini leo, licha ya kuwako na dawa zilizo bora sana tulizowahi kutibiwa nazo, na dawa zilizo bora sana na hospitali zilizo bora sana. Na hata hivyo katika uvumbuzi wetu wote wa kisayansi, hata hivyo kuna maradhi mengi kuliko ulimwengu ulivyowahi kujua, kwa kuwa kuna dhambi zaidi na kutokuamini kuliko ulimwengu ulivyowahi kujua. Tusaidie usiku wa leo, Tabibu Mkuu, na uwaponye wagonjwa walio miongoni mwetu.

Na utupe Roho, Roho wa kweli wa Krismasi. Wakati leo…kwamba wakati ambapo sherehe za kipagani, miti ya Krismasi inaabudiwa, hadithi za uongo za m—mtu anayeitwa Baba Krismasi, na sungura wetu wa Pasaka, na mitindo mbalimbali ambayo ulimwengu wa kibiashara umeitumia kwa faida yao, jalia iwekwe kando, Mungu. Jalia tuingie katika Kristo Neno, kwa kuwa tuliomba katika Jina Lake na kwa ajili ya utukufu Wake. Amina.

9 Kama mtafungua pamoja nami kwa ajili ya kusoma katika Maandiko Matakatifu, Luka Mtakatifu, mlango wa pili. Mnaweza kunisikia vizuri?

Je! Kuna mabadiliko yoyote katika maikrofoni? Mnaweza kunisikia huko nyuma sawa? Kama unaweza, inua mkono wako. Asanteni. Mlango wa 2 wa Injili kulingana na Mtakatifu Luka.

> *Siku zile amri ilitoka kwa Kaisari Augusto ya kwamba iandikwe orodha ya majina ya watu wote wa ulimwengu.*
>
> *(Orodha hii ndiyo ya kwanza iliyojulikana…hapo alipokuwa liwali wa Shamu.)*
>
> *Watu wote wakaenda kuandikwa, kila mtu mjini kwao.*
>
> *Yusufu naye aliondoka Galilaya, toka mji wa Nazareti, akapanda kwenda Uyahudi, ... mpaka mji wa Daudi, uitwao Bethlehemu,* (kwa kuwa yeye ni wa mbari na jamaa ya Daudi:)
>
> *Ili aandikwe pamoja na Mariamu mkewe, ambaye amemposa, naye ana mimba.*
>
> *Ikawa, katika kukaa huko, siku zake za kuzaa zikatimia,*
>
> *Akamzaa mwanawe, kifungua mimba, akamvika nguo za kitoto, akamlaza katika hori ya kulia ng'ombe, kwa sababu hawakupata nafasi katika nyumba ya wageni.*
>
> *Na katika nchi ile ile walikuwako wachungaji wakikaa makondeni na kulinda kundi lao kwa zamu usiku.*
>
> *Malaika wa Bwana akawatokea ghafula, utukufu wa Bwana ukawang'aria pande zote, wakaingiwa na hofu kuu.*
>
> *Yule malaika akawaambia, Msiogope; kwa kuwa, tazama, nawaletea habari njema ya furaha kuu, ambayo itakuwa kwa watu wote.*
>
> *Kwa maana leo katika mji wa Daudi amezaliwa Mwokozi, ambaye ni Kristo Bwana.*
>
> *Na hii ndiyo ishara kwenu; mtamkuta mtoto mchanga amevikwa nguo za kitoto, amelala katika hori ya kulia ng'ombe.*
>
> *Mara walikuwapo nanii…Mara waliku-…pamoja na huyo malaika, wingi wa…jeshi la mbinguni, wakimsifu Mungu, na kusema,*
>
> *Atukuzwe Mungu juu mbinguni, Na duniani iwe amani kwa watu aliowaridhia.*
>
> *Ikawa, malaika hao walipoondoka kwenda zao mbinguni, wale wachungaji waliambiana, Haya, na twendeni mpaka Bethlehemu, tukalione hilo lililofanyika, alilotujulisha Bwana.*
>
> *Wakaenda upesi, wakamkuta Mariamu, na Yusufu, na mtoto mchanga amelala horini.*
>
> *Walipomwona wakatoa habari waliyoambiwa juu ya huyo mtoto.*
>
> *Wote waliosikia wakastaajabu kwa hayo waliyoambiwa na wachungaji.*

*Lakini Mariamu akayaweka maneno hayo yote, akiyafikiri moyoni mwake.*

*Wale wachungaji wakarudi, huku wanamtukuza Mungu na kumsifu kwa mambo yote waliyosikia na kuyaona, kama walivyoambiwa.*

Bwana na aongeze baraka Zake katika kusomwa kwa Neno Lake.

10 Sasa, ni ninii … Kwa nini tukio hili kubwa lilifunuliwa kwa wachungaji? Hilo lingekuwa ni jambo la kushangaza kwetu. Nina baadhi ya Maandiko yaliyoandikwa hapa, na maandishi machache ambayo nitajaribu kuyasoma, kuwaelezea kwa nini kadiri niwezavyo. Na labda basi baada ya jambo hili, kwamba Bwana kwa neema Yake, usiku wa leo, ataondoa hizi ni kwa nini kutoka kwetu. Lakini alifanya … Karibu sisi sote, nadhani, wakati mmoja ama mwingine, tumeshangaa ni kwa nini tukio hili kubwa kuliko yote lilifunuliwa kwa wachungaji. Kwa nini lilifunuliwa kwa wachungaji na si kwa wanatheolojia wa siku hiyo? Hao ndio waliofunzwa kulisikia. Na ni kwa nini lilikuja na kuwapita matajiri, na kuwajia maskini? Pia, kwa nini liliwapita waliosoma na wenye hekima, na kuwajia wanyenyekevu na wasio na elimu? Kuna maswali machache ya kwa nini katika jambo hili.

11 Na sababu nyingine ninayoweza kusema, angalia, mtoto huyo mchanga alizaliwa Bethlehemu. Ambayo Bethlehemu katika tafsiri ya Kiebrania, kama tulivyokuwa nayo miaka michache iliyopita hapa, Bethlehemu maana yake ni "nyumba ya mkate wa Mungu." Nasi tulithibitisha katika Maandiko, Yeye asingeweza kuja mahali pengine popote. Bethlehemu ilianzishwa na Rahabu na nanii wake—mume wake. Rahabu alikuwa ni kahaba ambaye jemadari alimpenda, kutoka kwa—kwa jeshi la Israeli, baada ya kuiteka Yeriko. Na kwa imani aliamini Ujumbe wa Mungu, katika hali yake, naye akaokolewa. Na kutoka hapo, wakati Yoshua alipogawanya nchi ambapo kila mmoja angekuwa, …

12 Na kuna somo kuu ambalo wakati mwingine natumaini kuwa na uwezo wa kuleta huko Tucson, kuhusu hao mama wa Kiebrania wanaowazaa watoto hao. Wakati alipougua katika utungu wa kuzaa mtoto mchanga, aliita jina la mtoto huyo mchanga na hiyo ikamweka mahali pake katika nchi ya ahadi, kabila lake. Jambo kubwa, Neno lote la Mungu huafikiana moja kwa moja. Lisipoafikiana, Neno la Mungu silo lisiloafikiana, mawazo yako ndiyo ambayo hayaafikiani na Neno. Yote yanalingana.

13 Kwa hiyo, basi, Yeye alikuwa Mkate wa Uzima, kama tulivyofundisha juma lililopita huko Phoenix, ama juma lililotangulia. Na kwa kuwa yeye ni Mkate wa Uzima, asingeweza kuja mahali pengine ila "nyumba ya mkate wa Mungu." Na hiyo ndiyo iliyokuwa ile ni kwa nini. Sasa, hapa, Yesu amezaliwa Bethlehemu, na Bethlehemu kulikuwako na sinagogi, viongozi wakuu wa kidini waliishi Bethlehemu. Daudi mfalme-mchungaji mkuu alizaliwa Bethlehemu, baba yake Yese alizaliwa Bethlehemu, babu yake Obedi alizaliwa Bethlehemu. Pia, huko nyuma kabisa, yeye alitoka Bethlehemu.

Na hapa, Yesu Mwana wa Daudi amezaliwa Bethlehemu, moja kwa moja chini ya vivuli vya makanisa makuu. Basi kama watu hao wamefunzwa, na wamekuwa wakimtazamia Masihi kwa miaka hii yote; miaka elfu nne, Masihi alikuwa ametabiriwa kuja. Na basi kama Masihi akizaliwa katika kivuli cha kanisa kuu, kwa nini iliwabidi kurudi moja kwa moja wakaingia milimani kwa kundi la wachungaji wasio na elimu na wasiofunzwa, kuleta Ujumbe huu mkuu, Ujumbe wa kwanza? Nao wakawaagiza wachungaji! Si wenye hekima na waliofunzwa, bali ni wachungaji. Ni jambo la ajabu, sivyo? Lakini hapana budi kuwe na sababu fulani mahali fulani … Kuna sababu, sasa hapana budi kuwe na jibu kwa nini! Na hakuna mtu ajuaye jibu ila Mungu. Yeye Ndiye anayejua jibu.

14 Sasa, kumbukeni, Masihi alikuwa tayari mjini, alizaliwa mjini, katika hori; moja kwa moja karibu na makanisa makuu ambapo kuhani mkuu … na makuhani wakuu, na wanatheolojia, na wenye hekima, na waliofunzwa, wote walikuwa pale wakimngojea Masihi. Naye alikuwa pale, moja kwa moja katikati yao! Lakini kwa nini basi walienda kwenye … huko kwenye milima ya Yuda kwa wasio na elimu, wasio na mafundisho, wasio na elimu, maskini kuliko wote? Alionekana kama mtu asiyefaa sana kwa kazi hiyo, kufunua Ujumbe na kuwatuma nje kuuleta Ujumbe.

Mnajua maoni yangu? Huenda yasifae kitu, bali nataka kutoa maoni yangu: ninaamini ni kwa sababu ya hekima ya Mungu, kwamba Yeye alijua wasingeupokea Ujumbe kama huo jinsi ulivyokuja. Haikuwa katika ladha ya elimu yao. Ilikuwa ni tofauti. Haikuwa vile walivyofunzwa kuamini Yeye angekuwa. Ilikuwa ni kinyume cha ufahamu wao wa kitheolojia. Mafunzo yao yote, elimu yao yote ilipitwa, ikawa bure. Ninaamini ni hekima ya Mungu iliyojua ya kwamba wasingeupokea Ujumbe kama huo.

15 Kwa hiyo Masihi alikuwa hapa, na hapana budi kuwe na mtu anayemtambua. Naye alijua wale ambao hawakuwa wamechanganyikiwa katika upuuzi kama huo. Angekuwa anaweza hata na zaidi kuupeleka ujumbe Wake kwa kundi lisilo na elimu, kuliko vile angaliweza kwa kundi lililochanganyikiwa ambalo lilikuwa limeshika njia za mwelekeo mkali hata hakuna kitu kingaliweza kuwageuza, si hata Neno la Mungu.

Na sasa, rafiki Mkristo, hebu niulize swali hili, kwa unyofu wote na upendo. Nashangaa tu kama Yeye angetenda tendo lile lile usiku wa leo, na kututumia sisi katika kizazi hiki Neno la ahadi lililoahidiwa kwa ajili ya kizazi hiki, nashangaa kama wanatheolojia wetu, na walimu, na wenye hekima, wasingeukataa

Ujumbe huo kama vile tu walivyofanya wakati huo? Mwanadamu habadiliki, wala Neno la Mungu halibadiliki. Yeye ni Mungu asiyebadilika, Yeye habadiliki!

16 Angalia, Malaika wakija na … Malaika wakija na kutoa Ujumbe wao kwa watu wa hali ya chini sana, wakati kulikuwako na watu pale zaidi (wazo la kidunia la) wenye sifa kuliko hawa wachungaji maskini, wasiojua kusoma. Mchungaji alikuwa mtu asiye na elimu kuliko mtu yeyote, hakuhitaji kujua kitu ila kuhusu kondoo wake tu. Hakuhitaji kujua hisabati. Hakuhitaji kujua jinsi ya ku—kugawanya atomi. Hakuhitaji usomi wowote. Ilimbidi tu kuwajua kondoo wake, hayo tu ndiyo aliyohitaji kujua. Na Mungu, Hekima kuu, na Chemchemi na rasilimali ya hekima yote, angemchagua mtu kama huyo (watu, hasa, kama huyo), na kuwapita wasomi wote waliofunzwa vizuri waliofunzwa kujua Hilo. Inaonyesha jambo moja, ya kwamba walifunzwa katika fani isiyofaa. Akiwapita watu wote mashuhuri wa nchi hiyo; kulikuwa na watu wa maana, walimu mashuhuri, akina kuhani mkuu Kayafa, watu wengine wengi mashuhuri, Waisraeli wote wenye elimu nyingi, madhehebu yote, na wanatheolojia wote wenye kujigamba, Mungu alimpita kila mmoja wao! Sasa, hiyo ni hekima ya Mungu.

17 Angalia, Mbingu za Juu sana zikiharakisha kuwaheshimu walio wanyenyekevu sana na wasio na elimu. Aliye Juu Sana wa Mbinguni alishuka kujitambulisha kwa walio duni sana wa dunia, akiwapita wote walio katikati apate kujitambulisha kwa wachungaji wa kawaida; akija kuwapa hawa wachungaji wa kawaida Ujumbe ulio mkuu sana wa nyakati zote. Kulikuwa na wajumbe wengi mashuhuri. Tungewazia juu ya siku ya Nuhu, na hao manabii, na—na makuhani adhimu, na kadhalika, walikuwako katika siku zilizopita. Watu mashuhuri walio na elimu, wafalme, viongozi wakuu, watawala, bali Huyu hapa anakuja akiwa na Ujumbe mkuu kuliko jumbe zingine zote. Ujumbe ulikuwa ni nini? "Masihi yupo hapa sasa!" Mnaona? Na kulijulisha hilo, Yeye aliwapita wote waliofunzwa, kuwajulisha wachungaji wanyenyekevu.

Wazia jambo hilo: makasisi wote, watu wote wa kanisa, walimu wote, mafundisho yote ya the—theolojia, fedha zote zilizokuwa zimetumiwa, makanisa yote, na mafundisho, na madhehebu, yote yalipitwa! Elimu yote waliyokuwa wametumia juu ya wamishenari wo—wote, na ushawishi wote wa kubadili dini, uanachama wote, na kila kitu walichokuwa wamewazia wamefanya kumheshimu Mungu, hata hivyo Ujumbe ulio muhimu sana kuliko zote uliwapita. Ajabu! Kwa nini? Mnaona?

18 Na angalia, si hayo tu, bali mahali pasipotarajiwa kabisa kwa tukio kama hilo. Wachungaji, sasa, ndio walioupokea Ujumbe. Na sasa angalia mahali Ujumbe ulipokuwa: katika mahali pasipotarajiwa kabisa ambapo mtu yeyote angeutarajia kuja. Nami nashangaa, usiku wa leo, kama tulikuwa tukiutazamia Ujumbe wa kweli wa Bwana Yesu, sijui kama ungekuwa katika kundi lisilotarajiwa, mahali ambapo palikuwa … ambapo ulimwengu mkuu, wenye utamaduni wa hali ya juu na kanisa siku hizi wangefikiri lilikuwa ni kundi la—la, loo, wazushi? Nashangaa kama hilo halingekuwa mahali ambapo tungempata? Mahali pasipotarajiwa, na kwa wasemaji wasio na sifa. Wachungaji hawakujua kitu juu ya kunena, ila tu kuwaita kondoo; vema, labda hiyo ndiyo sababu Huo ukaja.

19 Lakini kulikuwako na Neno lililoahidiwa. Angalia, ingewezekana hilo litendeke tena.

Uliwapita watu wote walio bora wa nchi. Uliwapita watu wote walio bora, na ukafunuliwa kwa watu wasi kitu. Watu wote walio bora waliokuwa wametunukiwa nishani za—za daktari wa uungu na—na saikolojia, na—na elimu ya hali ya juu, na makanisa makuu na kadhalika, vyote vilipitwa na kufunuliwa kwa watu wa hali ya chini. Ile hekima, hekima isiyo na kikomo ya Mwenyezi Mungu ilifanya jambo hilo, kuwajulisha Ujumbe ulio mkuu sana uliowahi kutokea, "Masihi sasa yuko duniani." Ni hekima iliyoje! Ingeweza tu kutoka kwa Mungu anayejua hekima! Hekima yote na elimu yote, na kila kitu, sasa vilitupiliwa mbali na kupitwa na hekima kuu ya Mungu. Ninaendelea kurudia hayo kwa sababu ninataka yaingie ndani kabisa. Yote yameharibiwa, haikuwa na faida yoyote. Yote yalipitwa kusudi hekima ya Mungu ionekane wazi, ya kwamba Mungu huchukua wasio chochote na kuwafanya watu mashuhuri.

20 Tungeweza kusimama hapa na kuzungumza juu ya Yohana. Tungeweza kusimama na kuzungumza juu ya Eliya. Hakuna mtu ajuaye mahali Eliya alipotoka. Yote wanayojua, alitokea tu kwenye tukio. Manabii huko nyuma katika nyakati zote, walikuwa watu wa maana. Lakini Mungu alichukua hilo kuninii…na kuyapita ma—maadili ya kanisa, na mafundisho, kufanya…kuonyesha ya kwamba Yeye ni Mungu. Yeye huchukua kitu ambacho si kitu, kufanya kazi nacho. Yeye huonyesha hekima Yake na Uungu Wake kwa kufanya hivyo, kwamba Yeye huchukua watu wasio wa maana. Wakati Yeye alipomfanya mtu kwa mara ya kwanza, alichukua tu bonge la udongo na kumfanya mtu kwa hilo. Ambapo hakukuwa na kitu ila udongo, bali Yeye alimfanya mtu. Na Mungu huchukua watu wasio na maana sasa, kufanya mambo makubwa fulani nao. Na mradi tunafikiri sisi ni watu wakubwa fulani, basi hatuwezi kutumiwa katika mkono wa Mungu. Hatuna budi kuacha yote tuliyojua ama kujifunza. [Ndugu Branham anasafisha koo lake — Mh.] (Samahani.) Kama yule Paulo Mtakatifu mkuu, alisema ilimbidi kusahau yote aliyopata kujifunza, kusudi amjue Kristo.

21 Elimu yao yote, mafundisho yao yote na kadhalika, yalikuwa yakiwaharibu kabisa. Mwishowe yalimkataa! Elimu ile ile waliyokuwa nayo kwa ajili Yake, kumwamini Yeye, iligeuka na kuwa adui Wake mkosoaji sana, na kumsulibisha!

Je! Unajua ya kwamba historia inajirudia mara kwa mara? Ni kweli inayojulikana. Ingeweza kutukia tena moja kwa moja karibu na sisi. "Loo," unasema, "Kama ningeishi wakati huo, …" Vema, sasa, kama unataka kujua yale ungalifanya wakati huo, angalia hali yako ya sasa; nawe unaweza kuona yale ungalifanya wakati huo, kwa maana hakika inaonyesha wazi.

22 Walifunzwa kuamini Neno Lake, na halafu wakati Neno Lake lilipothibitishwa mbele ya macho yao, walilikataa Neno lililothibitishwa. Wakati Mungu alipothibitisha yale angefanya, na akasema yale angefanya, na kuthibitisha yale angefanya, ndipo waligeuka na kumwita mtu huyu "pepo mchafu" (ambalo liliwalaani wote). Wazia yale yaliyotukia! Wazia kilichowasababisha; mafunzo yao yaliwafanya wasitambue Neno lenyewe lililofanyika mwili kwa siku yao; mafunzo yale yale waliyokuwa nayo katika shule zao, wakiwa na waalimu bora sana.

Nawe unasema, "Vema, tusingefanya hivyo leo." Walimu wao walikuwa hodari sana kuliko wetu siku hizi (bora, hasa, kuliko walimu wetu), nao walishindwa. Hawakuwa na madhehebu mia tisa na tisini na sita mbalimbali kama tulivyo nayo siku hizi. Walikuwa na kama matatu hivi. Na katika haya matatu, yafuatilie hayo matatu, wala hakuna moja ya hayo matatu lililotambua jambo Hilo! Inaonyesha tu ya kwamba yale mwanadamu afanyayo ni upumbavu kwa Mungu. Mnaona?

23 Sasa, wao walishindwa kulitambua Hilo. Sasa … Nao wangefanya jambo lile lile tena.

Mwanadamu … Nia ni nzuri, daima ni nzuri. Na mwanadamu kamwe habadilishi mwelekeo wake, habadilishi njia zake sana; ninazungumza juu ya mtu wa ulimwengu. Mwanadamu daima humsifu Mungu, mtu wa kidini, kwa yale aliyofanya, na daima akiwaelekeza watu kwa yale Yeye atakayofanya, halafu anapuuza yale anayofanya! Mnaona? Huyo ni mwanadamu tu, ameumbwa hivyo, daima amekuwa hivyo. Na ninyi wasomaji wa Biblia usiku wa leo mnajua ya kwamba hiyo ni kulingana na Neno, "kweli." Wao daima wanamsifu Mungu kwa yale aliyofanya, wakisema yale atakayofanya, na kupuuza yale anayofanya. Hiyo ni tabia tu ya mwanadamu.

24 Sababu ya wao kufanya hivi, waalimu, kwa maoni yangu sasa: walikuwa wamelifasiri Neno, maana wote waliamini katika Masihi ajaye. Israeli wote waliamini jambo hilo, wangali wanaliamini leo. Lakini sababu ya wao kutomtambua, Ujumbe Wake haukuwa kulingana na uwezo wao wa kidini. Wao…tafsiri waliyokuwa nayo ya Neno, Masihi kamwe hakujidhihirisha Mwenyewe katika njia waliyokuwa wametafsiri ya kwamba angejidhihirisha. Kwa hiyo, na kwa sababu hiyo, hawakumtambua Yeye kwa sababu haikulingana na tafsiri yao. Kama nilivyosema hapo awali, na ninasema tena, "Mungu hahitaji mtu ye yote kufasiri Neno Lake. Yeye hujifasiria Mwenyewe."

25 Sasa, Biblia inasema … Hebu niwathibitishie sasa ya kwamba hiyo ni Kweli. Isaya nabii, miaka mia saba na kumi na mitano kabla jambo hili halijatukia, nabii Isaya alisema, "Bikira atachukua mimba, naye atazaa mtoto." Hapana shaka ya kwamba kila mmoja katika wakati huo alifikiri binti yao angekuwa ndiye mwanamke huyo, kwa maana Isaya alisema jambo hilo. Lakini, mnaona, ilikuwa ni miaka mia saba baadaye. Lakini wakati … Mungu hakuhitaji mtu ye yote kufasiri Neno Lake, wakati atakapolifanya, ama jinsi atakavyolifanya. Yeye alisema angefanya hivyo, Naye alifanya hivyo!

26 Mungu aliahidi ya kwamba Yeye … katika Isaya, pia, ninaamini sura ya 28, kama aya ya 18. Na pia katika Yoeli 2:28, ya kwamba katika siku za mwisho, miaka elfu mbili iliyopita, Yeye angemwaga Roho Wake juu ya wote wenye mwili. Yeye alisema, "Wana wenu na binti zenu watatabiri. Vijana wenu wataona maono. Wazee wenu wataota ndoto." Na mambo ambayo Yeye angefanya, Isaya alisema, "Kwa midomo ya watu wenye kigugumizi na kwa lugha nyingine nitasema na watu hawa, na hii ndiyo Raha." Lakini wasingesikia. Walitikisa-tikisa vichwa vyao na kuipita. Yeye alisema, "Meza zote za Mungu zingejaa matapiko, wala hakutakuwa na kitu kilicho safi." Na kama hiyo si picha ya Yerusalemu, na kanisa la siku hiyo kwenye kuja kwa Masihi, ni picha leo vile vile. Inajirudia tu.

Sasa, wakati Mungu anaposema atafanya jambo fulani, Yeye alifanya jambo hilo. Haidhuru mtu mwingine yeyote anawazia nini juu yake, kile mtu ye yote asemacho, Mungu anaponena jambo fulani, Yeye anawajibika kulifasiri Neno hilo Mwenyewe. Na thibitisho Lake la Neno ndiyo tafsiri Yake Mwenyewe. Angalia, akithibitisha Ujumbe Wake wa Masihi. Yeye aliahidi yale Masihi angefanya atakapokuja. Na wakati alipokuja …

27 Hata wakati wale mamajusi wa mashariki walipoangalia chini upande wa kusini magharibi, kutoka mahali walipokuwa huko Babeli, nao wakaona nyota kuu. Je! ulijua hakuna hata chembe ndogo ya historia, popote pale, ambapo chumba chochote cha kuchunguzia (ambako hata waliweka wa—wa—wakati kwa nyota, watu mashuhuri ambao walizisoma nyota hizi)… Hakuna historia inayosema ya kwamba ye yote wao aliiona hiyo nyota hata kidogo. Kwa nini? Hawakupewa, hawakuwa wakitafuta vitu kama hivyo. Bali hawa mamajusi walijua kungekuwako na Nyota ya Yakobo itakayochomoza, nao walikuwa wakiitarajia, nayo ilipita tangu wakati Yesu aipozaliwa Bethlehemu…

Sasa, ninajua mapokeo yetu ya Kikristo, ni kama tu makanisa yetu, mambo yake ni shaghalabaghala. Unatoka unaenda hapa na kuona mamajusi wakija kumwabudu mtoto mchanga; hakuna kitu kama hicho

katika Maandiko. Miaka miwili baadaye walifika pale, wakipitia kwenye uwanda tambarare na kuvuka Mto Tigri. Kamwe hawakuja kumwabudu mtoto mchanga, bali kijana mdogo mwenye umri wa karibu miaka miwili. Kwa nini ilikuwa, wakati uo huo, Herode akawaua watoto wote tangu umri wa miaka miwili na kuendelea? Ili apate kumnasa Masihi. Mnaona, wao … Mungu alikuwa amethibitisha kwa Neno Lake.

28 Na hao mamajusi walipofika Yerusalemu … Ile nyota iliwaongoza kwenye mji mkuu wa kidini wa ulimwengu, Yerusalemu. Na mara walipoingia kwenye malango hayo, ile nyota (ya kimbinguni iliyokuwa imewaongoza) ilikataa kuwaonyesha tena. Huku na huko barabarani watu hawa wazuri, matajiri wenye ngamia wazuri waliopambwa, na kadhalika … huku na huku mitaani wakisema, "Yuko wapi Yeye aliyezaliwa Mfalme wa Wayahudi. Tuliona nyota Yake mashariki." Na makao hayo makuu ya kidini, baada ya miaka miwili ya Ujumbe wa mchungaji, bado hawakuwa na jawabu wala kujua lolote juu Yake. Mkuu wa madhehebu yote hakuwa na jibu.

Kwa hiyo ikasumbua Baraza la Wazee, nao wakaita Waandishi waje wasome. Nao wakasoma hadithi ya Mika, nabii ambayo ilisema, "Nawe Bethlehemu, hu mdogo kamwe katika majumbe wote wa Yuda (mdogo kuliko wote), lakini kwako atatoka mtawala atakayewachunga watu Wangu, Israeli." Na baada ya Maandiko kusomwa (na bado yanathibitishwa mbele ya macho yao), bado hawakulikubali, ingawa Maandiko yalisema hivyo. Nina shaka sana wangefanya hivyo leo, kama Maandiko yaliyoahidiwa kwa ajili ya siku hii yangedhihirishwa. Huenda nisiwahubirie tena, bali ninawataka mpate hili. Bado wasingeamini!

Hekima kuu ya Baba inaifanya hekima ya binadamu kuwa ya kipuuzi sana hata Yeye humdunisha mtu. Kwa kweli yeye anafikia mahali ambapo inamfanya mwanadamu aone aibu sana juu yake mwenyewe, na yeye si mkubwa vya kutosha kukubali ya kwamba yeye "amekosea." Yeye angali anadumu na hadithi yake, haidhuru Baba atathibitisha jinsi gani ya kwamba Neno Lake ni kweli naye anafanya yale tu aliyoahidi kufanya. Mwanadamu anafikiri hekima yake ni bora sana kuliko ya Mungu, kama haiji kulingana na hekima yake, "Mbona, siyo hivyo." Hiyo ni kweli katika kila wakati, ingali inafanya hivyo. Mnaona jinsi jambo hilo lote lilivyoafikiana, sasa?

29 Ni uvuvio wa ulioje kwa wale wachungaji! Malaika wakishuka kuja kuzungumza na wachungaji, Malaika wa Mungu wakija kuzungumza na kundi la wachunga kondoo.

Sijui kama umewahi kuwa na majaliwa ya—ya kuzungumza na mchungaji ama kuwa na mchungaji mmoja, kitambo kidogo? Kama ungeweza, si—sitaki kusema jambo hilo kwa sababu ya tamshi langu ninalotaka kusema baada ya muda kidogo, bali mchungaji hukaa na kondoo sana hata yeye hucheka kama kondoo (mlio wa kondoo), anazungumza kama kondoo, na ananuka kama kondoo. Hiyo ni kweli, kwa sababu yeye yuko pamoja na kondoo. Hilo tu ndilo analojua, ni kondoo wake.

30 Sasa, Neno la Kweli lililothibitishwa. Wakati hawa wachungaji, wanyenyekevu, watu wasio na elimu … Ni heshima iliyoje, jinsi inavyofaa kwa mchungaji kupokea ujumbe wa kondoo aliyezaliwa upya. Isingeweza kuwa kitu kingine ila mchungaji. Hiyo ndiyo sababu Yeye alizaliwa katika hori, na si katika nyumba. Kondoo hawazaliwi katika nyumba, au katika chumba cha hospitali kilichopambwa kwa rangi ya waridi. Mnaona? Wanazaliwa katika banda, na makondeni.

Hiyo ndiyo sababu Yeye aliongozwa Kalvari. Huwezi kumfanya kondoo atembee kwenye njia kuu kwenda machinjioni. Je! Ulijua jambo hilo? Huko machinjioni, wana mbuzi anayewaongoza kondoo. Na wakati anapofika mahali pa kuulia, anaruka na kuwaacha kondoo waendelee. Kondoo hana budi kuongozwa, hawezi kujiongoza mwenyewe. Kwa hiyo, basi, ilibidi iwe ni mchungaji akiwajia nanii…kondoo wake. Wakati walipompata mtoto-Mungu huyo mahali pale pale yule mjumbe aliposema Yeye angekuwa, na wakati walipoupata Ujumbe huu wa mjumbe katika hori, mahali pale pale hasa Malaika aliposema Yeye angekuwa.

31 Sasa, niliwasikia watu wakisema, "Malaika alinena nami, Yeye alisema, 'hivi na hivi.'" Ni upuzi jinsi gani wakati mwingine; nami nimewasikia watu wakisema ya kwamba Malaika alinena nao, na kuwaambia "hivi na hivi" jambo ambalo lilikuwa ni kinyume kabisa na Neno. Sasa, Malaika angewezaje kufanya jambo hilo? Isingewezekana kabisa. Na kama Mungu alikuambia jambo fulani litatukia (unasema Yeye alikuambia hivyo), na halitukii, basi haikuwa ni Mungu akinena nawe. Kumbuka tu, hiyo ni kweli. Mungu hasemi uongo. Yeye hapatikani katika uongo.

32 Walipompata Mtoto huyo mchanga, ilikuwa ni furaha iliyoje kwao. Kwa sababu Malaika aliyewapa ujumbe huo, waliyakuta mambo jinsi hasa Malaika alivyosema yangekuwa, na mahali tu ambapo Malaika alisema ingekuwa. Hilo lilikuwa ni jambo lililoje kwao!

Katika hori, kwa nini? Mnaona jinsi hawa wachungaji walivyokuwa na raha hapo kwenye hilo zizi? Unafikiri mwanatheolojia angekuwaje mle ndani? Angeliweka pini puani mwake, na kusema, "Nitoe mahali hapa." Mnaona? Angekuwa mahali pasipofaa sana, angekuwa katika mateso.

Lakini, mnaona, ilikuwa "nyumbani tu" kwa mchungaji. Mungu anajua mahali pa kutuma Ujumbe Wake. Mnaona? Sawa kabisa. Katika hali hii wachungaji walikuwa ndani wakati huo, katika zizi lao pamoja na

Mwana-Kondoo wao, Ujumbe uliothibitishwa ambao walikuwa wameusikia. Ni zuri iliyoje! Mbele za Masihi, Neno lililothibitishwa la Ujumbe wao. Wakati wachungaji waliposikia ya kwamba Masihi alikuwa yupo duniani, nao wakaja uweponi Mwake, moja kwa moja katika mazingira yao wenyewe hasa, (na wakakuta kwamba ule Ujumbe ulikuwa ni kweli, ulikuwa umethibitishwa pale) jinsi jambo hilo lilivyowafanya watu hao wajisikie, kuona kwamba Mungu alikuwa amewafanyia jambo hili kubwa.

33 Mbona, wanachuoni wasingekuwa mahali hapo sana, chini ya hali kama hizo, wangeondoka upesi sana. Kwa nini? Yule Mjumbe akija kwa wachungaji wa kawaida. Labda hata wasingeweza … haya … Baadhi ya wachungaji hawa huenda wasingeweza hata kuandika majina yao wenyewe, nina shaka sana. Mnajua wachungaji ambao Yesu aliwachagua wakati alipokuwa hapa duniani, kuwachunga kondoo Wake, "Wanipenda Mimi, Petro, kuliko hawa?"

"Naam, Bwana, Wewe wajua nakupenda."

"Lisha kondoo Wangu." Na Biblia ilisema ya kwamba Petro alikuwa mtu asiye na elimu wala maarifa. Bado tunawachagua wachungaji.

34 Washiriki wa kanisa wa siku hizo zilizopita, na makuhani, na jamii iliyofunzwa vizuri katika siku hiyo ingekuwa mahali pasipofaa katika zizi. Sasa, sina hakika sana ya kwamba wengi wenu wangeweza kufahamu (labda, ninyi watu wa jijini) vile zizi la Kiyahudi lilivyonuka, vile lilivyoonekana, kama wanyama katika zizi hilo, na jinsi lingalikuwa. Mbona, baadhi ya watu hawa wa siku hizi wasingekuwa mahali hapo sana, hata—hata wasingeingia mlangoni. Lakini ilimpendeza Mungu, kwa hekima Yake isiyo na kikomo, kuwafunulia Hilo wale ambao wangelipokea. Wasomi, na watu wenye hekima wa siku hiyo bila shaka wasingeupokea. Wangefedheheshwa sana kuonekana mahali kama hapo.

Mbona, kwanza, kama wangalirudi kanisani mwao, na wangeshuhudia ya kwamba walihudhuria mkutano kama huo, na kuamini kundi la wachungaji wasio na elimu wakileta tukio kama hilo, wangefukuzwa kanisani mwao. . Wangefukuzwa kutoka kwenye jamii ya Bethlehemu, kama wangekutwa wakisikiliza kundi la watu wasio na elimu kama hawa wachungaji walivyokuwa. Bila shaka wangekuwa, wamefedheheka. Kama wangalishirikiana na watu wa kawaida, na wakiwa … wakikubali uzushi kama kuamini ya kwamba Mungu angeleta Ujumbe Wake kwa kundi la wachungaji wasio na elimu, wakati walikuwa wameandaa kila kitu kwa ajili yake. Wangalipoteza ushirikishwaji wao, ingaliwabidi kurudisha vyeti vyao, na wasingeweza kutambulikana miongoni mwa shirika la makundi yao ya siku hiyo; kwa sababu walikuwa wameshirikiana na kitu kama hicho, wala sio na watu wenye akili nzuri zaidi.

35 "Unathubutuje!" kuhani angesema. "Unakuja hapa madhabahuni pangu na uongo kama huo, na upuuzi kama huo, ati mtu fulani wa mwituni asiye na elimu huko nje ambaye haninii…hakwenda…hakupitia shule ya msingi. Na ungeamini ujumbe kama huo, ya kwamba, 'Malaika alishuka akaja akazungumza nao'?"

Lakini vipi kama mtu huyo angesema, "Niliona Ujumbe wake ukithibitishwa"?

Angesema, "Hebu upesi nikupe vyeti vyako. Na tokeni kwenye jumuiya hii!" Nyakati hubadilika, bali watu hawabadiliki. Labda ingetukia tena leo hii, wangetupwa nje ya makanisa yao.

36 Lakini wachungaji walijisikia vizuri kabisa mahali hapo pamoja na Mwana-Kondoo wa Mungu. Na mchungaji ye yote mzuri hufanya jambo lile lile. Wakati mchungaji mwema juu ya kondoo anapoweza kuona Neno la Mungu likifanywa dhahiri na kuthibitishwa, juu ya yale aliyoahidi kufanya, mchungaji huyo yuko moja kwa moja nyumbani. Sijali mtu mwingine yeyote anasema nini, kuna "Mungu aliliahidi jambo Hilo, na Mungu alilitimiza."

Wanasema, "Siku za miujiza zimepita. Hakuna kitu kama Ubatizo wa Roho. Hakuna kitu kama Ubatizo wa Roho Mtakatifu, huo ulikuwa kwa ajili ya mitume."

Lakini hebu mchungaji wa kweli wa Neno ahubiri Hilo, katika nguvu za ufufuo, ya kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele! Petro alisema katika siku ya Pentekoste, "Ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa hao walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie." Popote anapoita, ahadi hiyo na baraka hiyo ni ya kweli. Na hebu mchungaji halisi anayewalisha Neno aone hilo likithibitishwa, wanatheolojia wote ulimwenguni hawawezi kumnyang'anya Hilo; kwa kuwa anajua Mungu alisema jambo hilo, nalo linatukia. Hivyo tu. Ni Neno la Mungu tu daima. Neno Lake lilifanyika mwili na lilikuwa likikaa miongoni mwao, nao hawakujua.

37 Yeye aliahidi jambo lile lile katika siku hii. Sijui kama tungelitambua? Wenye kiburi na hekima hawakuwa wamepokea kitu kama hicho. Nao waliamini kama kulikuwa na kitu kama Masihi duniani, Yeye hakika ingembidi kuja kwa madhehebu yao. Ingekuwa ni kundi lao wangeipokea, ama "Haikuwa sahihi." Sasa, hebu wazia tu kwa makini. Kama haliko kwenye kundi lao, basi… Je! Mliona, basi? Mungu kamwe hakuchagua yeyote kutoka kwenye kundi lao, bali Yeye alichagua wale wasiokuwa na uhusiano wowote na lolote la hayo. Kwa sababu kundi moja lingesema, "Mnaona kile tulichofanya?" Nao wangefanya vivyo hivyo leo. Lakini Mungu huchagua watu wasio na cheo, hiyo ndiyo sababu alimchagua mchungaji. Wachungaji walikuwa nyumbani kabisa pamoja na mwana-kondoo Mungu miongoni mwao, Neno Lake

lililofanyika mwili miongoni mwao. Wenye kiburi na hekima kamwe hawakumpokea, aliwapita.

38 Nasi tungeweza kusema vivyo hivyo leo, ama katika wakati wowote. Ilikuwa ni mambo yale yale katika siku za Martin Luther. Jambo lile lile katika siku za John Wesley. Ilikuwa ni mambo yale yale katika siku za Wapentekoste. Lakini Mungu hazuiliwi na dhehebu la mtu yeyote! Yeye hutenda kazi na Roho Wake moja kwa moja kuthibitisha Neno Lake! Ilibidi liwe na lije katika tabaka la baraza lao wenyewe la sivyo wasingelipokea. Kama vile walivyo wakaidi sana leo, makanisa yote, hata wanaenda "kufanya hivi-na-hivi, na kuunganisha makanisa yote pamoja." Kama wanamtarajia mjumbe sasa, ambaye anaweza kuunganisha Waprotestanti wote, Wakatoliki na Othodoksi, kila kitu pamoja, waunde kanisa moja kuu.

39 Sasa, ndugu, nimekuwa na majaliwa ya kuwahubiria mamia ya dini mbalimbali, na kuna watu wazuri katika hizo zote. Lakini sasa, mnakumbuka, ninatabiri, "Kila dhehebu halina budi kukubali jambo hili, ama sivyo halitakuwa dhehebu tena. Ni kulazimisha." Je! mlisoma gazeti la Tucson leo ambapo makasisi wa Kikatoliki wanasaidia kuweka mhudumu, katika gazeti…wanasaidia kuweka mhudumu, huko Missouri, kasisi wa Kiprotestanti? Na ni akina nani walikubaliana na jambo hilo? Wapresbiteri, Wabaptisti, Waluteri, na Assemblies of God. Liko katika gazeti la Tucson leo.

Loo, linatisha! Si huyo mtu aliye mle ndani, ni hao viongozi wa makanisa, viongozi watawala wanaogeuza kitu hicho mle, mfumo unaokutupa ndani yake upende usipende. Huwezi tena kuwa dhehebu na uepuke hasira hii inayokuja juu ya nchi, nawe utaona kama hilo si kweli. Huenda nikawa nimeondoka wakati jambo hilo litakapotimia, rejeeni kwenye moja ya hizi kanda. Na halafu kama haikuwa hivyo, mimi ni shahidi wa uongo. Kama ndivyo ilivyokuwa, mimi nimesema Kweli.

40 Wangeliita "namna fulani ya matendo ya pepo mchafu" dhidi ya mawazo yao mazuri. Unasikia mengi sana leo kuhusu mawazo mazuri: unaweka tu nia yako juu ya jambo lolote, na kuwazia jambo zuri juu yake. Ibilisi anaweza kufanya hivyo! Kuna kitu kimoja tu kinachotawala yote, na hicho ni Neno la Mungu. Kama unafikiria kinyume cha Neno, sahau mawazo yako. Fikiria juu ya Neno.

"Masihi," walidhani, "asingepatikana mahali kama hapo, mchafuko kama huo."

Ungeweza kuwazia kuhani mkuu mzuri, mashuhuri, ama kasisi, akiwa amesuguliwa sawasawa katika theolojia, angeshuka aje kwenye zizi lililojaa samadi? Na kukubali Ujumbe wa maskini, mchungaji mnyenyekevu ambaye hakuwa na elimu, na angekuja na kusema "Unaona, ninaweza kukuthibitishia, huyu ndiye yule Mwana, huyu ndiye yule Mjumbe"?

Nanyi mnajua yale watu hao wangesema? "Mtu huyo ni mwaminifu, yeye ni mwaminifu sana katika yale anayosema, bali amekosea kabisa!"

41 Nimeona watu wakiishi maisha mazuri sana mpaka watu wasingeamini, wasingesema neno juu yao, bali wanasema "Yeye ni mwaminifu makosani. Kamwe yeye hajui yale anayozungumzia. Yeye hajui tu yale anayonena. Mungu, Yeye asingefanya jambo kama hilo."

Lakini hapa walikuwa na ushahidi! Na baada ya ushahidi, "Nendeni kule juu zizini mwone kama yule mtoto mchanga hayuko pale."

Wangesema, "Umelogwa na pepo fulani mchafu, ambaye amekufanya useme hivyo." Hata hivyo ilikuwa ni kulingana na Neno la Mungu! Nao walikuwa vipofu sana wasingeweza kuliona, kwa sababu theolojia yao ilikuwa imewapofusha. Ni msiba ulioje!

"Unashikwa mahali kama hapo? Katika machafuko kama haya yalivyokuwa? Katika zizi?" Wakati walikuwa na mahali pake pazuri pa kuja, walikuwa wameandaa kila kitu kwa ajili Yake kuja, halafu kuwazia ya kwamba angeshuka (na kwenda) na wala asiwaletee walimu wao Ujumbe huo. "Na ungewapa kundi la wachungaji wasio na elimu? Halafu amlete Mwanawe Mwenyewe, na kumfanya azaliwe katika zi—zizi? Zizi la banda la kawaida? Vema, katika—katika hori la majani makavu? Mbona, isingaliwezekana!" Wasingeliamini, kwa sababu lilikuwa nyenyekevu sana.

42 Na ni rahisi sana, hivyo ndivyo wenye hekima daima wasivyolitilia maanani. Ni rahisi sana, linawashangaza. Walimtazamia Mungu huko mbali, wakati Yeye yupo papa hapa. Mnaona? Wanatafuta jambo fulani huko ng'ambo, wakati liko papa hapa pamoja nao sasa: Kristo, amefufuka katika wafu, yeye yule jana, leo, na hata milele.

Mambo yao yote makuu yalipitwa. Lakini hakika ilikuwa ni Kweli, ya kwamba "huyo hapo Masihi." Tunajua jambo hilo leo. Tunaamini jambo hilo leo. Tunalikubali leo.

Lakini kama Mungu aliahidi jambo fulani kwa ajili ya Krismasi hii, aliahidi jambo fulani kwa ajili ya siku hii, na kuthibitisha ya kwamba ndivyo ilivyo, na tungali tunaliacha, tuko tu katika tabaka lile lile walilokuwa (huko nyuma kwenye siku hiyo) hao waliolikwepa; kwa sababu halininii—haliji katika ladha yetu ya kimadhehebu. Hiyo ndiyo sababu tuko katika mchafuko mwingi sana kwenye Krismasi hii.

43 Yesu Kristo hajafa, Yeye yu hai. Yeye yuko hapa leo! Biblia ilisema, "Ni yeye yule jana, leo, na hata

milele." Yeye alisema, katika Yohana Mtakatifu 14:12, "Yeye aniaminiye Mimi …" (si yeye anayejifanya ananiamini, yeye asemaye ananiamini) "Yeye aniaminiye mimi, kazi nizifanyazo mimi yeye naye atazifanya. Na zaidi ya haya atafanya, kwa sababu mimi naenda kwa Baba." Nami nimemwona, katika maisha yangu mwenyewe, akifanya kiasi kikubwa zaidi cha kazi zile zile (alizofanya wakati huo) kuliko zile zilizoandikwa katika kurasa za Biblia hii. Na linapita juu ya kichwa na wenye hekima leo, na kufunuliwa watoto wachanga wanaoweza kujifunza; kama vile Yesu alivyoomba. Ni kweli, amefanya mengi kuliko Yeye … Nimeona katika siku yangu, ya miaka yangu thelathini na mitatu ya huduma, nimemwona Yeye akifanya mengi kuliko yale nimesoma Yeye akiyafanya katika Biblia; mengi zaidi ya jambo lile lile.

44 Lakini haidhuru Yeye alifanya nini basi, unafikiri Baraza la Wazee lilimwamini? "Vema," wakasema, "umelogwa." Lakini, tuchunguze, mahali walipokosea ilikuwa ni kujua … katika kutafuta, si yale kanuni zao za imani zilisema, bali yale Neno lilisema Masihi angefanya katika siku zao. Na hapo ndipo tunapofanya kosa leo, si kuyachunguza Maandiko. Yesu aliwaambia, "Yachunguzeni Maandiko, ndani yake mnafikiri mna Uzima wa Milele, na ndiyo yanayonishuhudia Mimi. Wanakwambia Mimi ni nani."

45 Angalia, Mungu alijua tangu zamani wangefanya jambo hili, hiyo ndiyo sababu tu ilimbidi kulichukua kwa wachungaji. Alijua wasingefanya jambo hilo, wasingelipokea. Sasa mnaona ni kwa nini ilibidi iwe ni wachungaji? Kwa nini wachungaji? Wanatheolojia wasingelipokea. Kwa nini wachungaji tena? Je, lingekuja kinyume na Neno Lake? La! Walikuwa ni wachungaji, waliwajua kondoo; na hivyo ndivyo alivyozaliwa, kondoo, mwana-kondoo. Angalia, Yeye alikuwa Mwana-Kondoo. Walikuwa—walikuwa ndio pekee ambao wangemkubali. Mchungaji ndicho kitu pekee ambacho kingemkubali Mwana-Kondoo. Walijua jinsi ya kumchunga, na ndivyo ilivyo leo tunapoupata Ujumbe wa Mwana-Kondoo.

46 Sasa jambo la kushangaza! Mtu aliye mnyenyekevu sana, asiye na elimu akimsujudu Imanueli kwenye zizi. Ninii … Na kulikuwa na watu huko nje, siku zile zile, wakifundisha theolojia yao. Umati mkubwa, wakitoka kila mahali, kutoka kote nchini, walikuja kutoa sadaka ambazo Yehova alisema "zilinuka sana katika pua Yake." Na hapa kulikuwako na wachungaji wanyenyekevu, katika zizi, wakimwabudu Imanueli; Mungu Mwenyewe alifanyika mwili, na amelala katika hori. Mnaona, jinsi ambavyo sisi tukiwa na kisomo chetu kikuu, na kichwa chetu kimerudishwa nyuma kana kwamba tunajua jambo fulani, na Mungu anakipita kitu hicho chote. Mnaona? Yeye hufanya yale anayoahidi kufanya, na Yeye daima hufanya hivyo. Lakini wazia juu ya hawa wachungaji wa hali ya chini huko nje sasa wakimsujudu Imanu- … Imanueli katika zizi. Inashangaza sana. Hakika ni kweli!

47 Kisha kutoka … Baada ya wao kumsujudia, na kutambua ya kwamba Ujumbe ambao walikuwa wakihubiri ulikuwa umethibitishwa, hao hapo … walikuwa wametoka wakimsifu Mungu kwa Ujumbe wa ajabu sana wa Malaika. Sasa linganisha jambo hilo na siku hizi. Simameni tu kidogo na kuwazia. Mwanadamu huko nje akimsujudu Mungu, na kumsifu kwa yale waliyokuwa wameona, yale waliyosikia, yale waliyojua kwamba ni Kweli, wakiwa na Ujumbe usioaminika kwa mtu mwenye elimu. Ilikuwa ni kinyume cha mawazo yote ya kikanisa, na hata hivyo ilikuwa ni Kweli! Ni Kweli! Waliliamini. Na sasa, hekima ya mwanadamu inawezaje kuwa upumbavu! Halafu wakisema ya kwamba kwaya ya Malaika iliwaimbia noeli ya kwanza. Ungeweza kuwazia jambo hilo? Huyo ni mchungaji ambaye hangeweza kuandika jina lake, akinuka kama zizi la kondoo, akitembea barabarani, akipiga makelele, "Utukufu kwa Mungu Aliye juu sana! Tunajua ya kwamba Yeye yuko duniani!"

Yule kasisi akasema, "Mtu huyo amerukwa na akili. Angalia vitabu hivyo uone kama yeye ni mshiriki wa kusanyiko letu. Yeye hakika anatutia aibu kwa mafundisho yake yasiyo ya kimaadili. Mwondoleeni mbali nasi. Hatutaaibishwa miongoni mwa watu."

Vema, unaweza kuaibika miongoni mwa watu na kutukuzwa mbele za Mungu; ama kuchukua chaguo lako, maana, kumbuka, ladha ya kidini ya siku hii hailingani na Neno la Mungu. Hakuna ladha mia tisa na sitini na tisa mbalimbali Zake. Ni ladha moja, Neno moja, Mungu mmoja. Hivyo tu.

48 Wakisema ya kwamba Malaika waliwaimbia noeli ya kwanza, na pia wakisema ya kwamba "walipata Ujumbe kutoka kwa Malaika." Malaika aliwatokea, akawapa Ujumbe, nao wakaenda wakagundua Ujumbe huo ulikuwa ni Kweli. Na kusema, "Mbali na hayo, Malaika alituimbia noeli ya kwanza."

"Ungeweza kuwazia?" Wanasema, "Maskini jamaa huyo." Hakukuwa na jambo kama hilo kutokea miongoni mwao, wajua, kwa hiyo kwa namna fulani lilikuwa ni fundisho la kigeni kwao. Na hiyo ndiyo sababu hawakuweza kulipata katika Maandiko, haikuwa kwao kulipata. Haiwezekani kwa wenye hekima, hakuna tukio kama hilo lililowahi kuwapata. Haiwezekani, bali hata hivyo ilikuwa ni Kweli. Ni Kweli, tunajua ni Kweli. Wazia! Waongofu wa kwanza wa Kristo na kusanyiko la kwanza walikuwa wachungaji, si makasisi; wachungaji, wachungaji. Kwa nini wachungaji?

49 Angalia! Huko nje wakimsifu na kumtukuza Mungu kwa yale waliyokuwa wameona na kusikia, waliwasikia Malaika wakiimba kwa mara yao ya kwanza kwa mwanadamu. Malaika hawakuwa wamewahi kumwimbia mwanadamu hapo kabla. Na hebu ziangalie hizo kwaya, jinsi walivyokuwa wamesimama na kuzizoesha na kuzifunza sauti hizo, "wangeimba wakati huo wa kuzaliwa kwa Masihi," nao wote walipuuzwa! Nao Malaika walishuka na kumwimbia mchungaji wa kawaida wa kondoo, si kwa mavazi ya

makasisi, bali wakiwa wamevaa nguo za wachungaji. Basi angalia ni nani aliyepata Ujumbe wa kwanza, ni jambo lisilowezekana.

Na mahali hapo ambapo ulitolewa, si katika makanisa makuu, bali nyikani, huko nje nyikani ambako Malaika wa Bwana alikuja. Si katika kanisa, jangwani. Hata hakukaribishwa kanisani. Walifikiri alikuwa, nao walifikiri walikuwa nao, bali Mungu alithibitisha ya kwamba ilikuwa ni makosa. "Yeye anaweza kutoka katika mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto." Hiyo ni kweli.

50 Mara ya kwanza Malaika walipowahi kuimba kwenye sherehe, ilikuwa ni Mbinguni. Kama utaangalia katika Ayubu 38:7, (kama ninavyoona baadhi yenu mkiandika), wakati Mungu alipopanga kwanza kuumba uumbaji Wake wa kwanza, dunia. Ayubu alikuwa mtu mashuhuri, mwerevu, naye alikuwa na kila namna ya hekima. Yeye alisema, "Ninapoenda sokoni, vijana hao wakuu, wote wananisujudia, na wanataka tu hekima yangu kidogo." Naye hakuweza kujua ni kwa nini ilimbidi atendewe jinsi alivyotendewa.

Na kwa hiyo Mungu akamwuliza, kasema, "Jifunge kama mwanamume, kwa sababu ninashuka kuja kuzungumza nawe." Na wakati Mungu aliposhuka katika upepo wa kisulisuli, Yeye alisema, "Ayubu, ulikuwa wapi kabla sijaiweka misingi ya nchi? Wakati nyota za asubuhi zilipoimba pamoja, na wana wa Mungu walipiga makelele kwa furaha, ulikuwa wapi basi, Ayubu?" Naye alikuwa amekata tamaa wakati huo. "Ulikuwa wapi?"

Mnaona, mara ya kwanza Malaika walipowahi kuimba kwenye sherehe, ilikuwa ni Mbinguni. Lakini mara ya kwanza walipowahi kuimba duniani, ilikuwa ni kwa wachungaji katika kuzaliwa kwa Mungu, Imanueli duniani; wanadamu wa kwanza waliopata kumsikia Malaika akiimba, walikuwa ni wachungaji wanyenyekevu.

51 Tunapowachukua wanawake wetu waliopakwa rangi, kukata nywele zao, kuvaa kaptura, na kuzungushia aina fulani ya joho la kanisa, na kuwasimamisha na kuimba kama kitu fulani, halafu tunafikiri ya kwamba Mungu hana budi kusikiliza hayo? Yeye ana Malaika huko nyuma ambao wanaweza kumfurahisha tangu … kabla hajaumba mwanadamu. A-ha. Toka uende ukaishi … na uvae nguo ambazo ni chukizo kwa Mungu, na unawezaje kutarajia hilo kuwa ni la Mungu? Unasema, "Vema, mimi ni wa …"

"Ulikuwa wapi nilipoiweka misingi ya nchi? Niambie ambako niliikazia. Iko wapi ekseli zinazoizungukia? Ulikuwa wapi wakati huo?" Unafikiri inambidi Mungu kutuomba sehemu ya hekima yetu. Hekima yetu ni upumbavu tu Kwake. Yeye hufanya yale anayosema atafanya.

52 Sasa angalia, Mungu anajiandaa kufanya uumbaji mwingine. Yeye kuumba nchi inayopita, uhai upatikanao na mauti. Malaika wanaimba Mbinguni. Lakini hapa Yeye anaumba Uzima mpya, Uzima wa Milele kwa mwanadamu, Naye anawaimbia raia Wake kupitia Malaika; duniani, si Mbinguni. Mbinguni kulikuwa na Uzima wa Milele. Mnaona? Naye aliimba…waliziimbia Mbingu, wakati kuumbwa uhai upatikanao na mauti kulipoingia, na hapa uumbaji usiopatikana na mauti unaingia, na sasa wanawaimbia watu wa duniani. Mara ya kwanza, kwa wachungaji. Inashangaza, sivyo?

53 Alikuwa ameanzisha kiumbe kipya. Ilikuwa ni kitu gani? Uumbaji Wake Mwenyewe. Mungu alifanyika mwili akakaa kwetu. Hiyo ni … Biblia ilisema, "Katika mwanzo wa kuumba kwa Mungu." Mungu aliumbwa katika umbo la mwanadamu; katika Yesu Kristo, Mwanawe, Mungu aliishi. Yeye alijenga maskani Yake ya nyama na mifupa, na kuishi katika maskani hiyo; Mungu, Imanueli, "Mungu pamoja nasi." Yeye alijijengea nyumba, apate kuishi ndani yake, kusudi aweze kuakisi Neno Lake kwa raia Wake kupitia jambo hilo. Mnajua Mungu ni nini, Mnapomwona Kristo.

54 Kumbuka, daima kuna kuimba wakati wa kuzaliwa kwa mfalme. Ni wangapi walijua jambo hilo? Bila shaka, ulifanya hivyo. Vema, sasa, unafikiri kama Mfalme huyu angezaliwa kule chini, mwanamke angekuja mbio kwenye kanisa kuu mahali fulani, na kusema, "Andaa kitanda upesi sana, na uwapate madaktari, kwa sababu atamleta Imanueli duniani"? Maskini mwanamke kutoka Nazareti, mji ulio duni kuliko miji yote, ninii…mwovu kuliko Tucson ama yoyote ya hiyo mingine, na hata hivyo maskini mwanamke huyu yuaja mbio pale kwa kuhani mkuu mashuhuri na akasema, "Ni—ninajiandaa kumzaa Imanueli." Wangemtupa gerezani. Hakika wangefanya hivyo. Bila shaka wangefanya hivyo. Kwa uzushi kama huo kuletwa miongoni mwa watu wake, asingeweza kustahimili jambo hilo. Wala hata asingeweza leo. Lakini ni jambo lile lile tu linalotukia, vivyo hivyo tu.

55 Angalia, hapana budi kuwe na kuimba. Wafalme walikuwa … Asingeimbiwa. Watu wasingemwimbia, kwa sababu hawakumwamini. Na hiyo ndiyo sababu … Hili hapa linakuja, afadhali ulipate. Hiyo ndiyo sababu leo watu wanaona aibu kumsifu Mungu, wanamwonea Kristo aibu! Makanisa makuu hayatapokea Ubatizo wa Roho Mtakatifu, yamewekwa katika njia yao ya kikanisa hata hawatampokea. Mungu atamtafuta mtu fulani ambaye anaweza kujipatia sifa kwake. "Yeye katika mawe anaweza kumwinulia Ibrahimu watoto," ninapomnukuu Yohana tena.

Angalia, raia Wake hawana budi kumwimbia. Na raia Wake wakati huo walikuwa ni Malaika Wake, nao waliwaimbia wachungaji Wake ambao walipaswa kuuchukua Ujumbe Wake.

56 Ni nani wanaopaswa kuusikia kwanza? Bila shaka, raia Wake. Hao ndio ambao wangekuwa wa kwanza kusikia kuimbiwa kwa Mfalme, wangekuwa ni raia Wake. Na raia Wake walikuwa ni nini? Kwa namna fulani linashangaza, sivyo, ndugu? Haikuwa makasisi Wake. Haikuwa wanatheolojia. Hiyo ni kweli. Haikuwa watu wa kimadhehebu. La, ilikuwa ni wachungaji. Kwa nini? Kulikuwa na kondoo aliyezaliwa, hiyo ndiyo sababu. Mnaona? Raia wake walisikia, ambao Mungu alijua wangeamini. Mungu alituma Ujumbe Wake kwa wale ambao wangeuamini. Yeye ni hekima yote; Yeye anajua mahali pa kutuma Ujumbe Wake, ni nani atakayeuamini. Aliye juu sana wa Mbinguni alitumwa kwa mtu wa chini sana duniani.

Yesu alisema, katika Mathayo 5, "Heri walio maskini katika roho, kwa maana ufalme wa Mbinguni ni wao." Mariamu, katika … Kama mnayaandika hayo Maandiko, hayo ni Mathayo 5. Na kama mnaandika Maandiko … Hayo ndiyo niliyoandika hapa, ni Maandiko.

57 Mariamu alisema, katika Luka 1:52, wakati alipotiwa mafuta na Roho, Roho Mtakatifu akiwa juu yake, alisema, "Yeye amewakweza wanyonge." Mariamu alisema hayo, mama ya Yesu, alisema, "Yeye amewakweza wanyonge."

Luka pia alisema, "Watu wa kawaida walimsikia kwa furaha." Sio wa—wasomi, wa—wanatheolojia, madaktari wa sheria na wa uungu; bali watu wa kawaida walimsikia kwa furaha, watu wa hali ya chini.

Katika Maandiko yote matakatifu, Ujumbe wa ukombozi umetolewa na wachungaji na kupitia kondoo.

Sasa inanibidi kufikia ukomo, kwa sababu tunafikia wakati wa kufunga. Ninayaruka Maandiko mengi kusudi tu niweze kuwafikisha kwenye wazo hili.

58 Kote katika Maandiko, ukombozi umewakilishwa kupitia kwa wachungaji na kondoo. Hiyo ni kweli. Sote tunakubaliana na jambo hilo. Kwa nini? Ilikuwa katika kivuli na mfano. Na cho chote … Kama sijapata kuuona mkono wangu, nami niliangalia hapa chini kwenye kivuli cha mkono wangu, na ninaona nilikuwa na vidole vitano, ningejua ya kwamba huo ulikuwa ukiakisi; kivuli kilikuwa kikiakisi kilicho halisi. Na hiyo ndiyo sababu Ujumbe daima ulikuja kwa … ukombozi kwa kondoo, kwa sababu tangu mwanzo … Na ilikuwa kwa njia ya kondoo, na kwa wachungaji, kwamba Yeye alijifunua Mwenyewe. Yote ilikuwa ni vivuli na mifano.

59 Sasa hebu na tuangalie mwanzo. Adamu na Hawa, wakisimama pale mbele za Mungu kusikia Ujumbe Wake kwao, walikuwa wamejifunika viunoni mwao ngozi ya kondoo. Ujumbe wa kwanza uliopata kusikika, ulitolewa juu ya ngozi ya kondoo iliyokufa, ambayo Mungu alikuwa amechinja na kuwafunika Adamu na Hawa kwayo. Baada ya wao kujaribu kutengeneza dini yao wenyewe ya majani ya mtini, haingefaa kitu. Dhabihu ya kondoo ilikuwa imeanzishwa kwa ajili ya upatanisho tangu mwanzo kabisa, dhabihu ya kondoo.

Sasa, tutafunga jambo hili sasa, na kuwaonyesha ni kwa nini ilibidi wawe wachungaji; na kwa nini ilibidi iwe, ilibidi awe ni kondoo.

60 Sasa, manabii wa Agano la Kale walijivika ngozi za kondoo (tunajua jambo hilo, a-ha), wakionyesha imani yao katika Neno Lake la kuja kwa Mwana-Kondoo mkamilifu. Hiyo ndiyo sababu manabii.

Sasa, Neno la Mungu halimjii mwanatheolojia, hakuna … yeye—yeye ndiye anayelivuruga. Hiyo ni kweli. Hakuna kitu kama kusema kamwe … Wewe ukisema, "Vema, jamaa huyu ni mwanatheolojia." Hilo linamweka mbali sana na Neno kuliko chochote ninachojua. Mnaona? Neno la Bwana Mungu, Mungu asiyebadilika, kamwe halibadiliki. Mahali po pote katika Biblia, Neno la Mungu daima liliwajia manabii. Si kwa wanatheolojia ama madaktari, kwa manabii! Nao daima, kila wakati, walikataliwa na kupingwa.

61 Manabii kwa kawaida walikuwa ni wachungaji pia. Manabii walijivika ngozi za kondoo, kwa sababu walivaa ngozi ya kondoo waliowachunga. Na ujumbe wa kwanza, kwa ki—ki—kizazi kilichohukumiwa, kilikuwa juu ya ngozi za kondoo. Manabii, ninasema tena, walivaa ngozi za kondoo ambazo walijifunika nazo, maana walikuwa wakishuhudia kwa jambo hilo, ya kwamba waliamini ya kwamba Mwana-Kondoo mkamilifu alikuwa yuaja kwa ajili ya sadaka hiyo. Ndipo Neno la Mungu likawajia juu ya ngozi za kondoo. Hawa wachungaji … ama hawa manabii kwa kawaida walikuwa ni wachungaji. Ibrahimu alikuwa ni mchungaji. Isaka alikuwa ni mchungaji. Yakobo alikuwa ni mchungaji. Musa alikuwa ni mchungaji. Daudi alikuwa mchungaji. Wawakilishi wote wa Mungu kwa kawaida walikuwa ni wachungaji.

62 Sasa tutaenda kuona ni kwa nini uliwajia wachungaji. Walijua kondoo walikuwa hawajiwezi bila ya mchungaji wa kuwaongoza. Wao … kondoo hajiwezi kabisa, hawezi kwenda peke yake. Hiyo ndiyo sababu Mungu aliwafananisha watoto Wake wanaoamini na kondoo. Hawana budi kuongozwa. Lakini angalia kile kinachokuongoza! Usimpate mbuzi, atakuongoza machinjioni. Mungu kamwe hakutupa mbuzi, alitupa Mwanawe (Roho Mtakatifu) kutuongoza. Yeye ndiye Kiongozi wetu, si wachungaji wa kujibunia, bali mchungaji aliyetolewa na Mungu ambaye anawalisha kondoo kwa chakula cha kondoo.

63 Sasa, mchukue nguruwe, na umwambie nguruwe huyu, "Nitakufanya mwana-kondoo." Nawe unamwosha. Na upake rangi kucha zake za vidole vya mguu, na—na kadhalika. Na kumpa chakula kama kondoo, kumpa namna fulani ya—ya chakula. Na kumweka pale sakafuni ama nje kwenye … ambapo ka—

kundi la kondoo, kwenye shamba la alfalfa ama cho chote kile. Na kama kuna shimo la matope mahali po pote, nguruwe huyo ataenda moja kwa moja kwenye shimo hilo la matope awezavyo kwenda. Mnaona? Kwa nini? Ni kwa sababu asili yake ingali ni nguruwe.

Na hiyo ndiyo sababu washiriki wa kanisa, leo, wanajiingiza katika mambo ya ulimwengu, mnaona, ni kwa sababu tabia yao haijabadilishwa. Watakula aina yo yote ya maporomoko ya kidini, ya kitheolojia, bali Neno la Mungu hawawezi kulivumilia. Wataingia na kulisikiliza Neno …

64 Mwajua, mnafiki mkubwa sana ulimwenguni, ni kunguru wa kale. Katika Biblia, kulikuwako na wawili waliotoka safinani. Yule kunguru wa kale alitoka na hakurudi kamwe, kwa sababu yeye ni nderi, mla mizoga. Aliketi juu ya miili ya mizoga iliyokufa na akajaza tumbo lake kwa mzoga huo uliokufa. Lakini wakati alipomfukuza hua, hua asingeweza kustahimili uvundo huo, kwa hiyo akarudi nyumbani kwa Baba pamoja na Nuhu, na kupiga mlangoni mpaka Nuhu akamruhusu aingie.

Sasa, kunguru anaweza kuketi hapa nje na kumla farasi aliyekufa, siku nzima, na kuruka huko nje kondeni na kula nafaka pamoja na hua. Lakini hua hawezi kuruka kule na kula juu ya farasi aliyekufa, na kisha kula nafaka; ingemwua. Mnaona, hua hana nyongo yo yote, wala hawezi kumeng'enya.

Na wakati hua yeyote wa Mungu, hua yeyote anayekula Neno ama kondoo, mnyama safi, unapoenda kuwapa vitu vya ulimwengu, wao wanajua Bwana wao alisema, "Yeye anayeipenda dunia au mambo yaliyo katika dunia, kumpenda Mungu hata hakumo ndani yake." Ukimpa kitu kinyume na Neno hilo la Mungu, hawezi kulivumilia. Lakini ibilisi anaweza kuchukua Hilo na ulimwengu pia, na kuviita vyote ni vya Mungu. Huwezi kuchanganya mafuta na maji, hayatachanganyikana.

65 Wao, wachungaji hawa wote, walijua kondoo alikuwa mnyonge bila mchungaji. Nao walikuwa wachungaji, nao walijua ya kwamba hana budi kuongozwa.

Ni huzuni jinsi gani kuona, leo, kwamba wanajaribu kuwalisha kondoo, uchafu. Lakini kondoo hatakula. La, bwana! Mnaona, walikuwa wakijaribu kuwalisha kondoo, kule nyuma, uchafu. Na wakati Neno lilipokuja, walikuwa wamezoea sana uchafu, hawakujua Neno. Na hivyo ndivyo ilivyo leo, wakati jambo lile lile lilithibitisha na kuthibitisha ya kwamba Mungu angefanya jambo fulani. Ndipo wao wamezoea sana kula uchafu, na wamelishwa uchafu, hata u-…vema hakuna kuwazungumzia, kamwe hawatalisikiliza jambo Hilo, hivyo tu. Mbwa … Biblia ilisema, "Kama vile mbwa anavyorudi kwenye matapiko yake, na nguruwe kwenye kugaagaa kwake matopeni, vivyo hivyo nao."

Wanasikiliza Neno, kisha wanarudi moja kwa moja kwenye kule kugaagaa kwa kale! Na kusema, "Aha, ni ulokole. Usiamini kitu kama hicho."

66 Mungu … kondoo hufanya vivyo hivyo leo, hawana budi kuamini mlo wa Neno. Hawatakula chakula kingine chochote. Huwezi kuwapa mlo wa kikanisa, kondoo halisi. La! La! Nenda kawaambie, "Sasa angalieni, sote tutakuwa pamoja. Sasa, Yesu aliomba kwamba sisi sote tuweze kuwa 'mmoja.'" Mlisikia jambo lile lile kule Tucson si muda mrefu uliopita, siku chache zilizopita, bali ni uongo! Yesu kamwe hakuomba … Alifanyaje … Unawezaje kulifanya Neno lijihukumu Lenyewe, lijilipue Lenyewe? Basi Mungu si zaidi ya mtu mwingine yeyote.

Yesu alisema, "Watu wawili wanawezaje kutembea pamoja wasipopatana?" Utachukuaje Methodisti, Baptisti, Presbiteri, na Katoliki, na kuzitupa zote pamoja na wawe mmoja? Huenda ukawa mmoja chini ya kichwa cha mwanadamu, bali Yesu alisema, "Ili wapate kuwa mmoja hata kama—kama mimi na Wewe tulivyo mmoja." Sasa, Yeye anataka sisi sote tuwe kitu kimoja ndani Yake ambacho ni Neno! Amina! Hilo hapo, "Mmoja pamoja na Baba." Na Baba ni Mwana, ni yeye yule. Na ni Neno lile lile, Neno lililodhihirishwa, likijidhihirisha lenyewe katika siku hii kama lilivyofanya katika siku nyingine yoyote, kusudi upate kuwa mmoja.

67 Angalia, Yeye alisema, "Kama vile Baba alivyonipeleka Mimi, mimi nami nawapeleka." Baba aliyemtuma, aliingia ndani Yake kuthibitisha Neno. Na Yesu yeye yule anayewatuma watu Wake, anaingia katika watu anaowatuma; na kusema, "Kazi nizifanyazo Mimi, ninyi nanyi mtazifanya." Hakika, Yeye aliomba kwamba tupate kuwa mmoja; mmoja pamoja Naye, si mmoja na madhehebu. Si mmoja na mfumo fulani, bali mmoja na Mungu. Kwa kuwa Mungu katika Neno Lake ni Mmoja, na Yesu na Mungu walikuwa Mmoja, na wewe na mimi na Neno hatuna budi kuwa mmoja. Hiyo ni kweli. Hatuna budi kuwa mmoja katika kukubaliana na Neno. Si yale mtu mwingine asemayo, hii si tafsiri ya kibinafsi. Lichukue, vile lisemavyo, na uliamini; naye Mungu atalithibitisha, na kuthibitisha ya kwamba ni kweli. Unafikiri ni kwa ajili ya mitume tu, chukua Neno Lake kwa ajili ya jambo hilo, uende ukalijaribu wakati mmoja na uone. Utaona ya kwamba litafanya kazi kwa ajili yako vile vile tu Yeye alivyoahidi. Naam, bwana!

Hawatakula kwenye matope, hawana budi kula chakula cha kondoo. Yohana Mtakatifu 10 inatangaza ya kwamba, "Kondoo Wangu wanaijua Sauti Yangu." Na kama Yeye ni Neno, basi ana Sauti ya aina gani? "Kondoo Wangu wanaijua Sauti Yangu, wageni hawatawafuata." Mnaona? Yesu alisema, "Hawakuifuata sauti ngeni." Kwa hiyo, kondoo Wake hawafuati sauti ya mgeni. Hawatawafuata.

Manabii, wachungaji, na kondoo, wote wanashuhudia juu ya kuja.

68 Sasa mwone Mungu asiyebadilika katika mipango Yake isiyobadilika ya Neno Lake siku hii. Sasa hebu wazia tu dakika chache: Neno lisilobadilika.

Sasa angalia! Kama—kama Musa angekuja na ujumbe wa Nuhu, haungefaa kitu. Kama Yohana Mbatizaji angekuja na ujumbe wa Musa usingefaa kitu. Kama Yesu angalikuja na ujumbe wa Musa ama wa Nuhu, haungefaa kitu. Na Wesley akaja na ujumbe wa Luther, haungefaa kitu. Kama Pentekoste ingekuja na ujumbe wa Wesley, haungefaa kitu; tulisikia tu jambo hilo likishuhudia. Sasa, Mungu anaendelea tu kusonga mbele. Angalia tu Neno, mnaona mahali tulipo.

69 Basi kwa nini wasitangaze tangazo la kwanza la wachungaji … Kama manabii hawa wote, watu hawa wote wakuu walikuwa wachungaji, basi ni kwa nini Mungu (Yule asiyebadilika) abadilishe mtindo Wake papa hapa, na kuuleta kwa wanatheolojia? Ilikuwa ni wachungaji. Kule kuwasili kwa Mwana-Kondoo mkamilifu, lile toleo la dhambi, kunapaswa kuja kwa mchungaji.

Mchungaji anawajua kondoo wake vizuri zaidi kuliko mtu mwingine yeyote. Hakuna mtu anayewajua kondoo kama vile mchungaji, yeye amefunzwa kuwajua. Pia walijua ni aina gani ya chakula watakachokula. Wao … yeye alijua kile kondoo wangekula, naye anawajua kondoo wake kwa kile wanachokula. Ninii … ungemwona kondoo akienda kwenye kibanda na kuanza kula uchafu, ungesema, "Mwondoe huyo mla mizoga." Mnaona? Kwa hiyo Mungu alijua mahali pa kuwatuma.

70 Sasa hebu na tumwite mmoja wa manabii-wachungaji wakuu wa Yehova, kuthibitisha ya kwamba Mungu alikuwa katika manabii hawa waliovaa ngozi ya kondoo. Angalia sasa. Tutamwita, kwanza, Musa. Hebu tumwangalie. Huduma Yake itatuonyesha Yehova katika nabii-mchungaji Wake. Sasa, tutachukua tu labda moja, kama tuna wakati, kwa kama dakika kumi zifuatazo. Tutachukua wawili wao, lakini labda hili litakuwa sawa.

Musa; Yehova anajionyesha Mwenyewe hapa, katika nabii-mchungaji huyu. Yeye alipewa karama tatu kuthibitisha huduma yake na kuwaita wazee wa Israeli, na kwa Farao. Angalia huyu nabii-mchungaji, sasa. Yeye huwapa, daima, manabii Wake, ishara ya kimbinguni, kuthibitisha ya kwamba ilikuwa ni Mungu ndani yao; kwa kuwa hakuwezi kuwa na uwepo wa Mungu bila mambo ya kimbinguni kutukia. Kamwe Yehova hajawahi kutokea bila ya kimbinguni kumfuata. Haina budi kuwa hivyo. Kwa hiyo Yeye daima alijithibitisha Mwenyewe kwamba alikuwa pamoja na hawa manabii, kwa kuthibitisha yale waliyokuwa wakitabiri, kama ilikuwa ni kulingana na Neno Lake.

71 Sasa, ishara ya kwanza—ya kwanza aliyompa … huyu nabii-mchungaji (angalia), aligeuza fimbo yake kuwa nyoka.

Pili, mkono wake ukageuka ukoma.

Tatu, kuchukua maji kutoka kwenye Mto Nile huko Misri, na kuyageuza kuwa damu.

Sasa, Yeye alimpa ishara tatu kuithibitisha Misri, na pia kwa Israeli, ya kwamba alikuwa Neno lililonenwa na Mungu.

Sasa, kumbukeni, Musa aliita katika uumbaji! Hiyo ni kweli. Alichukua mchanga na kuutupa juu hewani, na kusema, "Viroboto na waje," na viroboto wakaja. Kasema, "Nzi na waje," ndipo nzi wakaja. "Vyura na waje," nao vyura wakaja. Yeye alileta katika uumbaji! Sasa, mwanadamu hawezi kuumba, bali kwanza haikuwa ni mwanadamu. Ilikuwa ni Yehova katika nabii-mchungaji Wake! Amina!

72 Angalia! Ishara ya tatu aliyompa haikuwa na uhusiano na kazi yake, wala haikuhusiana na nafsi yake; ishara yake ya tatu. Angalia, ishara mbili za kwanza zilihusiana naye, yeye mwenyewe na kazi yake. Na ndizo zilizokuwa ishara mbili pekee ambazo Biblia inasema kwamba "zilikuwa na sauti." Ile ishara nyingine haikuwa na sauti. Lakini zile ishara mbili zilizotolewa kutoka kwa nafsi yake, na kwa watu wake, zilikuwa na sauti. Lakini ishara ya tatu, sasa angalia, ilitolewa … ishara, ishara ya tatu, ilikuwa ni ishara ya mauti: maji yakigeuka kuwa damu. Kama ninii yako—kama ninii yako—kama damu yako ingegeuka kuwa maji, basi ungekufa. Na ambapo kuna damu, damu iliyomwagika, ni ishara ya mauti; ndivyo ilivyokuwa kwa Farao. Ya tatu ilikuwa ni kuyageuza maji ya Nile kuwa damu, yalikuwa ya kuonyesha—kuonyesha Ujumbe wake kwa Farao kwamba Mungu wetu ni Mungu juu ya Nile, juu ya mungu wa Nile. Yeye ni Mungu juu ya kila kitu, Naye ataleta mauti kwa taifa hilo. Na hivyo ndivyo hiyo ishara ya damu ilivyokuwa. Loo, jamani! Ishara ya moja kwa moja ya mauti: damu!

73 Lakini hizo zingine mbili zilikuwa na sauti za unabii. (Na—na—natumaini mnasoma sasa, kati ya mistari, yale ninayosema.) Lakini zile ishara zingine mbili zilikuwa na sauti za unabii kwa Israeli kuhusu wakati wao ujao. (Sasa kwenu ninyi mliokuwa huko mlimani si muda mrefu uliopita, wakati ule mwamba ulipotupwa juu.)

Sasa, na kwenda … alikuwa anaenda kubadilisha maumbile, kuyafanya yatimie kwao. Angalia hiyo

nguzo, mwangalie yule nyoka, angalia Bahari ya Shamu, na chochote alichofanya, sasa. Angalia hiyo fimbo ya mchungaji ikiwatengenezea njia ya kupitia. Fimbo hiyo iliyokuwa mkononi mwa mchungaji, ilikwepa kila kipengee cha theolojia na mambo yote makuhani waliyokuwa wamesema, na fimbo hiyo ya mchungaji iliwaongoza kotekote kupitia kwenye kila kitu kisichowezekana (kwa mwanadamu). Wakati Farao alipojaribu kuwazia ya kwamba "maporomoko ya maji yalifoka huko juu ya milima na kutupa maji, ndipo yakayafanya yageuke kuwa damu," ndipo Mungu akanyesha moto kutoka mbinguni. Naye akanyesha mvua ya mawe kutoka mbinguni, na Yeye—Naye akanyesha chawa juu ya nchi, na kila kitu.

74 Yeye alifanya nini? Kwa fimbo hiyo ya mchungaji, si ki—kitabu cha kiada, si wazo la mwanatheolojia, bali fimbo ya mchungaji! Tunalifikia katika dakika moja; fimbo ya mchungaji, Yeye alifanya hivyo. Si kitabu cha maombi cha—cha kimadhehebu, bali fimbo ya mchungaji. Fimbo ya mchungaji akiwaongoza kondoo wake, akiifanya njia iwe wazi walipokuwa wakienda kwenye Neno lililoahidiwa nchini. Hicho ni kitu kizuri jinsi gani leo cha Fimbo ya Mchungaji, leo, ikiwaongoza kondoo Wake kwenda kwenye ile Nchi ya Ahadi; ikikwepa theolojia zote na kitu kingine chochote cha ulimwengu huu, na mambo ya ulimwengu, na madhehebu, kila kitu; ikifungua njia, na kuthibitisha Neno Lake kuwa ni Kweli; Fimbo ya Mchungaji ikitangulia.

75 Na tazama, fimbo ile ile ya mchungaji iliyokuwa ikiwaongoza kondoo … Unaamini jambo hilo? Hakika aliwaongoza kondoo, aliwakomboa kutoka Misri akiwa na fimbo hiyo mkononi mwake. Tungeweza kusema mengi zaidi juu yake. Lakini kufikia kwenye upeo wake, yeye aliwaongoza kondoo na akatuma hukumu juu ya waliokataa Huo! Fimbo ile ile ambayo inakuwa baraka kwa mmoja, inakuwa laana kwa hao wengine. Maji yale yale (ya mahubiri ya Nuhu) yaliyomwokoa, yaliuhukumu ulimwengu. Fimbo ile ile iliyoongoza Israeli kwenye nchi ya ahadi, iliwahukumu wale waliokataa kumfuata nabii-mchungaji. Hiyo ni kweli, ikawa fimbo ya hukumu.

Maumbile; angalia jinsi Mungu anavyonena katika asili Yake. Kama tu tungalikuwa na wakati. Niliandika maandishi pale: Mungu akinena katika asili Yake. Hatuna wakati wa kulithibitisha.

76 Lakini kuthibitisha baadaye, kwa njia ya yule nyoka wa shaba juu ya konzo la kondoo la mchungaji (ambalo alimzungushia nyoka huyu, huko nyikani), hili linazungumzia juu ya upatanisho wa kweli ukija kwa ajili ya magonjwa na dhambi.

Hiyo fimbo yenyewe ilikuwa imegeuka kuwa nyoka mbele ya Farao, na Farao yule yule alijaribu kuiga kwa kutumia wachawi. Na vivyo hivyo na Farao wa siku hizi za kisasa, na wanaojifanya waaminio, waigaji wa kimwili wa Ujumbe, wanajaribu kuiga jambo lile lile bila kujua mahali linakotoka; na kuliingiza katika kitu fulani cha kimadhehebu, wakati Liko huru kwake kama hewa isivyoweza kuzibwa. Hakika! Lakini jaribu kuiga, fanya uigaji.

Lakini, angalia, fimbo hii hii ya mchungaji iliwala nyoka wengine. Hao nyoka walikuwa wapi? Walikuwa ni fimbo sakafuni, na kulikuwa na fimbo moja tu iliyoinuliwa. "Mbingu na nchi zitapita," alisema Yesu, "bali Neno Langu halitapita." Ananena juu ya upatanisho wa kweli unaokuja kwa ajili ya dhambi.

77 Pia, wakati ujao wa Israeli ulitoa … na pale ambapo nilinena juu ya Israeli, sasa katika siku zijazo … Huko walipewa ukombozi kutoka katika utumwa wa mauti na nabii-mchungaji. Walitolewa kwenye utumwa na nabii-mchungaji mwenye fimbo. Mnaona? Ilikuwa ikinena juu ya Mkombozi wa Israeli wa baadaye, kutoka mautini na kuzimu, kwa Nabii Mchungaji ambaye tutazungumza habari zake.

Sasa, kwa yote hayo … wote kama tujuavyo Israeli, hawakulipokea Neno la nabii-mchungaji, Israeli wote hawakulipokea. Sasa, angalia, walikuwa wakilalamika. "Loo," wakati alipokuwa akifanya miujiza, "alikuwa ni mtu mashuhuri," lakini ilipofikia Ujumbe wake, "hiyo ilikuwa ni tofauti." Ishara zote kuu zinafuata ujumbe mpya unaokuja. Tunajua jambo hilo. Huko nyikani walilalamika, huko nyikani, na wakafa kwa maelfu. Kusema kweli, hakukuwa na wawili pekee waliopata kupita ambao waliokolewa kutoka katika watu milioni mbili na nusu, wawili kutoka katika milioni mbili na nusu.

Mnasema, "Hiyo … Ni jambo gani lililowapata?" Wamepotea Milele.

"Wote, Ndugu Branham?" Yesu alisema hivyo.

Walisema, "Baba zetu walikula Mana jangwani, nao wakanywa kutoka kwenye Mwamba."

Naye … Yesu alisema, "Nao, kila mmoja wao, amekufa," wametengwa milele, mnaona, kila mmoja.

78 Angalia walilalamika juu ya njia iliyoandaliwa na Mungu, ndiyo sababu walikufa. (Sasa, kwa makini, msikose maneno haya machache ya mwisho.) Walilalamika! Kilichowafanya wafe nyikani, walilalamikia njia iliyoandaliwa na Mungu: kwa Ujumbe wa mtu mmoja, nabii, uongozi wa mtu mmoja. Niambieni ni wakati gani Mungu alipotumia kundi kuongoza. Hutalipata katika Biblia. Mtu mmoja, wao … Neno lilimjia Musa!

Kora; sote tunajua ya kwamba yeye—yeye alijikusanya pamoja na kulalamika juu ya Mungu kutokuwa mwenye haki, kufanya jambo kama hilo, kumfanya mtu mmoja na Ujumbe. Yeye alisema, "Sisi sote ni

watakatifu. Kwa nini hatuwezi kuwa na dhehebu? Na kwa nini hatuwezi kuwa na … kuanzisha hili, na kufanya hili, na kufanya lile?"

Mungu alimwambia Musa, "Jitenge naye, nimechoshwa na jambo hilo." Pia kumbukeni, Yuda ananena jambo lile lile, katika siku za mwisho. Hiyo ni kweli, "Waliangamia katika maasi ya Kora." Tunajua pia kile kilichompata Kora na wale—na hao wengine waliolihoji Neno la Mungu na hekima ya Mungu ya uongozi huo wa mtu mmoja: kila mmoja wao aliangamia.

79 Sasa, tutamwona Mungu katika nabii-mchungaji, akionyesha mipango Yake ya usoni katika sauti ya ishara inayofuata. Sasa, tazama. Tunaliona pale, sasa hebu na tuliangalie katika ishara inayofuata.

Sasa, angalia, alitumwa kwa ndugu zake katika utumwa, chini ya utumwa, akiwa na Ujumbe wa ukombozi, akiwa na ishara aliyopewa na Mungu kuthibitisha madai Yake. Israeli walitafuta Ujumbe wake, waliuamini, kila mmoja wao, lakini katika wakati wa jioni … Walienda kwa ajili ya miujiza yake, lakini katika wakati wa jioni wakati wao … yeye alitoa Ujumbe wake, "Ilikuwa ni tofauti." Wote ambao hawakuamini Ujumbe huo, walikufa. Hiyo ni kweli. Ujumbe ulikuwa ni nini? Ujumbe huo ulikuwa ni wa hukumu ijayo. Jioni, wakati wa jioni, Mungu alitoka akapitia kwenye kambi ya Israeli kuona kama watu walikuwa wameamini Ujumbe wa nabii-mchungaji Wake; na wote ambao hawakuwa wameuamini, waliangamia.

80 Sasa angalia, tutauleta kwa Mchungaji Mkuu katika dakika chache tu. Mnaona? Angalia huduma ya Mchungaji Mkuu-Nabii. Ya miujiza Yake, kila kanisa lilifunguliwa na lingempokea. Walitaka wagonjwa wao waponywe. Walitaka kufanya mambo makuu. Umaarufu wake ulikuwa mkubwa. Lakini wakati wa jioni ulipowadia, siku moja baada ya Yeye kugeuza maji kuwa divai, na kuwalisha maelfu, mkate, na kufanya miujiza, Yeye alianza kuketi chini na kuzungumza nao. Naye akawaambia, "Mimi na Baba Yangu ni mmoja. Kwa nini wasema, 'Tuonyeshe Baba'?"

"Loo, ndugu! Mtu huyu akijifanya sawa na Mungu?" Hilo lilikuwa ni zito sana kwa mawazo yao ya kidini. Bali ilikuwa ni Kweli, Yeye alikuwa! Mnaona? Lakini walipofanya hivyo, wengi hawakumfuata.

Ndipo akageuka na kusema, "Msipoula Mwili wa Mwana wa Adamu, na kuinywa Damu Yake, hamna Uzima ndani yenu."

Sasa, unafikiri mtu mwerevu, msomi angewazia nini? Nadhani makuhani waliokuwa wamemwalika hekaluni waliona—waliona aibu sana ku—kuwa Naye pale. "Kufikiri ya kwamba mtu angesimama na kusema jambo kama hilo, 'Msipoula Mwili Wangu, na kuinywa Damu Yangu.'" Wakasema, "Huyu ni kizuu mfyonza damu, mnaona, 'Kula Mwili Wangu na kuinywe …' Mbona, yeye ni mla watu. Ninyi watu wenye akili nzuri mtaninii … mtaachana na kichaa kama huyo."

Yeye hakulielezea kamwe, Yeye alilisema tu! Alifanya hivyo kuwakwaza, kuwatenganisha kondoo Wake na mbuzi. Alifanya hivyo kuwatupilia mbali. Na ndipo hakuna mtu aliyetaka kushirikiana Naye. Hawakuwa na ushirikiano tangu wakati huo na kuendelea. Mnaona?

81 Angalia, wakati wa jioni, Mungu alitoka akaenda kambini na kuona ni nani aliyeamini. Naye alifanya jambo lile lile katika siku za yule Mchungaji Mkuu. Angalia huduma ya Nabii Mchungaji Mkuu, lakini angalia jambo hili, kwa waaminio wa Ujumbe Wake, lakini si … Ujumbe huu wa jioni, wasingeuamini. Wasingeamini ya kwamba Yeye alikuwa ni Mungu. Walitaka kumfanya mtu mzuri. Walitaka kumfanya nabii. Alikuwa ni mtu mzuri, Naye alikuwa Nabii, bali alikuwa zaidi ya huyo. Hilo ndilo fundisho la kawaida leo, kwamba "Yeye ni mtu mzuri tu, alikuwa nabii." Yeye hakupungukiwa na Imanueli! Yeye alikuwa Mungu aliyedhihirishwa katika Yesu Kristo Mwanawe, akimfanya Yeye na Baba mmoja. Hilo tu ndilo Yeye angeweza kuwa.

82 Zekaria 14:7, huenda nikasema jambo hili, linazungumza juu ya Nuru za jioni na Ujumbe tena katika wakati wa mwisho. Mliona jambo hilo? Wote waliomfuata Musa, waliona ile Nguzo ya Moto iliyomtambulisha juu ya Mlima Sinai. Yeye alikuwa ameshuhudia, na kunena juu ya hii Nguzo ya Moto kuwa katika kichaka na alikuwa amemwambia Ujumbe huu, wengi wao hawangeuamini. Lakini wote waliomfuata kutoka Misri (waliotoka ulimwenguni na kuvuka bahari ya utengano, wakaenda nyikani), waliona Nguzo ile ile ya Moto (aliyonena habari zake) ikimthibitisha nabii mchungaji kuwa ndiye mchungaji wa kondoo. Waliiona, na wengi wao bado hawakuiamini baada ya kuiona.

83 Angalia jinsi, tena, Mungu asiyebadilika, yule Nabii Mchungaji Mkuu, aliwachukua wale waliokaa karibu Naye pamoja na huduma Yake kwenye Mlima wa Mizeituni; yule Mchungaji-Nabii Mkuu, Yule tunayenena habari Zake, Yesu. [Sehemu tupu kwenye kanda — Mh.] … Na kumsikia Baba (Nguzo ile ile ya Moto) ikimthibitisha, aliyemthibitisha Musa.

Mungu yeye yule ambaye Musa alinena habari zake, alimjia Musa na kuthibitisha kwa Nguzo ya Moto ya kwamba Yeye alikuwa Yehova aliyekuwa akimwongoza Musa. Mungu alikuwa katika nabii-mchungaji Wake.

Hapa Yeye anamchukua yule Mchungaji-Nabii mwingine, yule Nabii Mkuu, Kondoo Halisi, Yesu, na

kuwachagua watu watatu, na kuwachukua juu ya Mlima wa Mizeituni, na hapo akamthibitisha Yesu. Na hata alijitenga Mwenyewe kutoka kwa watu wengine wote, kasema, "Huyu ni Mwanangu mpendwa, msikieni Yeye!" Nao walipoinua macho yao, hawakuona mtu ila Yesu peke yake. Hiyo ni kweli. Yeye alikuwa Ndiye. Sasa, hilo latosha, nijuavyo mimi. Mnaona?

84 [Sehemu tupu kwenye kanda — Mh.] …?… [Sehemu tupu kwenye kanda.] …?… uso. Musa alikuwa mbele ya Shekina kwenye Mlima Sinai. Ilibadilisha uso wake. Wakati aliposhuka, ilimbidi ku—kuweka utaji juu ya uso wake, nabii-nabii Musa; ambaye Yehova alikuwa ndani, katika sehemu, sehemu tu, uso wake. Alikuwa na Neno kinywani mwake.

Lakini angalia wakati yule Mchungaji Mkuu alipokuwa mbele ya Shekina. Ilifanya nini? Ilibadilisha sura Yake yote. Yeye hakuwa tu sehemu ya Mungu, Yeye alikuwa ni Mungu! Alikuwa ni Imanueli.

Kwa nini ilibidi iwe ni wachungaji?

85 Angalia! Mnaona, sasa, Mungu Mwenyezi anafanya doria … akijionyesha Mwenyewe, hasa, katika Musa nabii mchungaji. Angalia jinsi Mungu alivyojitambulisha. (Hili ni tamshi langu la mwisho.) Kumwona, amesimama ametiwa mafuta mbele ya ile Nguzo ya Moto! Hakuna mtu mlimani kabisa ila Musa na Yehova. Amina! Amina maana yake ni "na iwe hivyo."

Angalia! "Weka mkono wako kifuani mwako!" Lakini, angalia ishara hii ya pili sasa ikiwa na sauti. "Weka mkono wako kifuani." Hatuna sababu ya kuamini ya kwamba Musa alitumia mkono wa kushoto, kwa hiyo hakuna budi aliweka mkono wake wa kuume kifuani mwake, maana watu wengi hutumia mkono wa kulia. Akaweka mkono wake wa kuume … Sasa angalia! Ni picha ya jinsi gani tunayoona hapa, ya Yehova katika nabii mchungaji Musa! Musa akimwakilisha Mungu, maana Mungu alikuwa ndani ya Musa. Mwangalie akiweka ninii yake … "Weka mkono kifuani mwako." Ni ishara iliyoje!

86 Sasa, huyo hapo amesimama, ameweka mkono wake wa kuume juu ya moyo wake (amesimama namna hii) ambapo siri za ukombozi zilikuwa zimefichwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu. Hii ndiyo sababu wachungaji. Yesu ni mkono wa kuume wa Mungu, sote tunajua. Huyo hapo Musa akimwonyesha Yeye hasa. Yeye alizishika siri za Baba, na ametuonyesha hizo. Angalia, mwangalie akivuta kutoka kifuani mwake mkono wake wa kuume umepigwa kwa ukoma wa kufisha. Ilionyesha kile Mungu angefanya kwa Mkono Wake wa Kuume. Angalia, ukoma hauna tiba. Angalia, tena, haikuwa tu ukoma wa kawaida, ulikuwa katika hatua yake ya mwisho, nyeupe kama theluji; mkono wake ulikuwa umepigwa na kitu cha kutisha. Jinsi ambavyo hapana budi Musa alijisikia wakati alipouvuta mkono wake wa kuume kutoka juu ya moyo wake, kutoka kifuani mwake, na mkono wake ukapigwa kwa ukoma! Ukoma unaonyesha dhambi, isiyotibika, na hasa katika hatua yake ya mwisho.

87 Na, ndugu, hapo ndipo ulimwengu ulipokuwa wakati Mungu alipouvuta Mkono Wake wa Kuume kutoka kifuani Mwake! Ulimwengu ulipigwa na ukoma wa kufisha, na hakuna tiba kabisa kwake. Ndivyo ilivyo usiku wa leo, kwa sababu hawatapokea dawa. Dawa ilitolewa pale Kalvari, lakini watu wanataka kuchukua maagizo ya kujibunia badala ya maagizo ya Mungu kwa ajili ya dhambi.

Angalia haukuja hatua kwa hatua, kama vile ukoma unavyofanya, lakini mara moja! Alipouvuta mkono wake, ulikuwa umepigwa, ulikuwa umejaa ukoma. Angalia yale Mungu aliyosema, "Sasa, hatua kwa hatua hutaingia dhambini; bali siku utakayokula, siku hiyo utakufa." Na hiyo ni kweli, "Siku utakayokula."

88 Angalia, nabii-mchungaji ndiye aliyejipiga. Alichukua, kwa amri ya Mungu, na akaweka mkono wake mwenyewe kifuani mwake, na kuutoa ukiwa umepigwa kwa ukoma. Nabii-mchungaji alifanya jambo hilo mwenyewe. Naye Nabii-Mchungaji Mkuu, Yesu, alifanya jambo hilo Mwenyewe, "Ninautoa uhai Wangu, hakuna mtu anayeutwaa kutoka Kwangu." Yeye alikuwa Mchungaji Mkuu, yule Nabii-Mchungaji Mkuu, "Hakuna mtu anayeutoa Kwangu, ninafanya hivyo Mimi Mwenyewe." Angalia haukuja pole pole, ulikuja kwa dakika moja. Yule Mchungaji Mkuu, Mwenyewe, alichukua hatia yetu na kujipiga Mwenyewe, akachukua dhambi zetu na kuziweka juu Yake. Si ajabu mshairi aliandika:

Huku miamba ikipasuka na mbingu zikiingia giza,  
Mwokozi wangu aliinamisha kichwa Chake na akafa;  
Pazia lililofunguka lilifunua njia  
Ya kwenda kwenye furaha za Mbinguni na siku isiyo na mwisho.

89 Siri hiyo ilikuwa katika kifua cha Mungu miaka hii yote, imefunikwa na mkono Wake wa kuume, Yesu. Mchungaji Mkuu alichukua hatia yetu kwa ajili yetu. Isaya 53:6, ilisema, "Alijeruhiwa kwa makosa yetu. Alichubuliwa kwa ajili ya uovu wetu. Adhabu ya amani yetu ilikuwa juu Yake. Na kwa kupigwa Kwake sisi tumepona." Siri ya uponyaji wa Mungu ilikuwa katika kifua cha Yesu Kristo, ama Mungu, Yeye alikuwa kwenye mkono wa kuume wa Mungu, huyo ndiye Kondoo pekee aliyeshikilia siri kifuani Mwake. Hiyo ndiyo sababu vivuli vyake vilipaswa kuwa kondoo daima! Wa kwanza alikuwa ni kondoo, wa mwisho alikuwa ni Kondoo. Hiyo ndiyo sababu ilibidi kumjia mchungaji, kujua jinsi ya kumtunza Kondoo wake. Mnalipata? Angalia, "Alijeruhiwa kwa makosa yetu, akachubuliwa kwa maovu yetu, adhabu ya amani yetu juu Yake."

90 Angalia, ulikuja upesi; na ukaondoka upesi, mara tu mkono wa kuume ulipotolewa kutoka kifuani mara ya pili. Ugonjwa huo mbaya ulikuwa umekwisha, alipouvuta mara ya pili. Na wakati yule Mchungaji Mkuu, Nabii-Kondoo, wakati aliposema … Kwenye msalaba wa Kalvari, wakati alipokuwa amelipa adhabu ya dhambi kwa ajili yetu sote, Yeye alisema, "Imekwisha." Dhambi ilikuwa imekwisha, adhabu ililipwa, madeni yalimalizika! Haikuchukua mwaka mmoja, ama hatimaye kuingia katika siku za mtengenezaji mwingine ama cho chote kile, ilikuwa imemalizika papo hapo!

91 Dhambi ilikuja mara moja, kwa kuvunja Sheria ya Mungu, kwa kuvunja Neno moja. Usiku wa leo, ndugu zangu, nafsi yako iko juu ya kuzimu kwenye mnyororo. Na mnyororo huo si mafundisho fulani ya kitheolojia, mnyororo huo si dhehebu fulani ama kanuni fulani ya imani unayoishi kwayo, mnyororo huo ni Neno la Mungu! Yesu aliwapa wanadamu Neno Lake wapate kuishi kwalo, na Hawa alivunja tu kiungo kimoja Chake kidogo. Na ninii … mnyororo wowote hauna nguvu kuliko kiungo chake kilicho dhaifu sana. Unapotoa Neno moja … Huo ulikuwa ndio mwanzo wa Kitabu.

Yesu alikuja katikati ya kile Kitabu, na kusema, "Mtu hataishi kwa mkate tu, bali kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu." Hiyo ilikuwa katikati ya kile Kitabu.

Mwisho wa Kitabu, Yeye alisema, "Mtu ye yote atakayeondoa Neno moja (kutafsiri Neno moja vibaya), kuondoa Neno moja kutoka Hapa, nitachukua sehemu yake kutoka kwenye Kitabu cha Uzima." Unapita kuzimu, ukining'inia kwenye Neno la Mungu. Usimwache mtu fulani akuingizie kitu fulani ndani yako ambacho si BWANA ASEMA HIVI!

92 Loo, ninaona … Vema, wanasema, "Hakika, yote tuliyofanya. Yote tuliyofanya!" Hilo ndilo ambalo labda makuhani wakuu na hao wengine walifikiri katika siku za yule Mchungaji Mkuu. Hivyo ndivyo Hawa alivyowazia. Hivyo ndivyo Shetani alivyomwambia, "Hakika Mungu hatafanya hivyo." Lakini Yeye alifanya hivyo, maana Yeye alisema angefanya hivyo. Na hiyo ndiyo sababu atafanya hivyo tena leo.

Si ajabu, kama alivyosema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ambapo watu wanane waliokolewa, kwa maji, ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu." Mnaona, ni wachache sana, "Kwa maana mlango ni mwembamba, na njia iendayo kwenye Uzima ni nyembamba, na ni wachache watakaoiona." Hiyo ni kweli. "Maana njia ni pana inayoongoza kwenye maangamizi, wengi wataipitia."

93 Wakati yule Mchungaji Mkuu alipopigwa, yule Nabii Mkuu wa Kondoo, wakati alipopigwa kule nyuma, Yeye alisema, "Imekwisha!" Na dakika hiyo, mara Mchungaji huyu alipopigwa, ilikuwa imekwisha. Dhambi ililipwa, hakukuwa na dhambi tena. Walikuwa safi, adhabu ililipwa. Waamini ambao majina yao yaliandikwa katika Kitabu cha Uzima, waliochaguliwa tangu zamani tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu, ilikuwa imekwisha dakika ile ile ambayo Yesu alisema imekwisha. Yeye, yule Mchungaji Mkuu, alikuwa amekuja kwa ajili ya kondoo Wake. Ilikuwa imekwisha, mkono wa kuume wa Mungu ulitolewa kutoka kifuani Mwake, ukapigwa. Ndipo kwenye Pasaka Yeye aliurudisha (amina), akauinua tena kifuani mwake, na kuusogeza chini kwako na kwangu, katika umbo la Neno Lake, apate kutukomboa kuturudisha kwenye bustani ya asili ambamo dhambi ilitutoa huko. Siri iliyofichwa ya moyo Wake mkuu ilifunuliwa na Nabii-Mchungaji. Ilifunuliwa na Mchungaji, Nabii-Mchungaji.

94 Si ajabu milima iliruka na kupiga makelele siku hiyo. Si ajabu jua liliuficha uso wake na kupaza sauti kwa furaha. Si ajabu maumbile yote yakafunguka; upepo uliitikisa miti hata ikatikisika na kutikisika, na kushangilia, na kuruka. Walimwona Nabii-Mchungaji, mlimani, akikomboa kila jina kwenye Kitabu cha Uzima. Nao waliona ya kwamba asili yao wenyewe ilikombolewa! Walipiga makelele, na kuruka. Na ulimwengu ukaingia katika tetemeko la nchi. Na milima ikapasuka, na miamba ikaanguka. Ndipo jua likatua. Na—na kila kitu kilitukia. Kama vile mkutano wo wote, wakati Mchungaji anapokufunulia ya kwamba "umekwisha!" Kuna …

95 Nimeona vipindi vya kuruka, na vipindi vya furaha, bali hapakuwapo na mtu yeyote aliyedhuriwa. Milima ilipiga makelele, nao…jua lilitua, na kila kitu kilitukia, lakini hakuna mtu aliyeumia. Nami nimeona mikutano ambapo nguvu za Mungu zilifunuliwa kwa watu ya kwamba wao "walikuwa huru na ulimwengu na mambo ya ulimwengu," na furaha ya Bwana ikalijaza kusanyiko. Walisimama na kupiga makelele, na kulia, na kupaza sauti kwa nguvu sana, kwa utukufu wa Mungu. Kamwe sikuona kitu cho chote kimakosa, walikuwa daima katika utaratibu; kwa sababu walikuwa wametambua hilo, jina lao lililokuwa limeandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Yule Nabii-Mchungaji mkuu alikuwa amewaletea Ujumbe, nao wakakombolewa, Nabii-Mchungaji. Haidhuru yale madhehebu mengine ya kikanisa yalisema nini juu ya jambo Hilo, walijua yaliyokuwa yametukia. Kama tu vile hao wachungaji walivyofanya huko nyuma, walijua yaliyotukia.

96 Hakuna mtu aliye na haki ya kuingia kwenye dawati takatifu kuhubiri Neno mpaka amefanya kama Musa alivyofanya, kukutana na Mungu, mwenyewe, juu ya mahali ambapo hakuna mwanatheolojia anayeweza kulielezea. Musa alikuwepo! Musa alikuwa pale! Haidhuru jinsi wajumbe wa Israeli walisema, "loo, ilikuwa ni upuuzi, uliwazia tu uliona hili; ni upuuzi," usingeweza kuondoa Hilo kwake, yeye alijua! Alikuwa pale! Lilitukia Kwake! Na hakuna mtu kwa di—digrii yake ya kitheolojia ama digrii fulani ya udaktari ana haki nyuma ya mimbara, kudai Ujumbe wa Yesu Kristo, mpaka kwanza amekutana na Mungu uso kwa

uso katika Nguzo ya Moto. Yeye hana haki ya kujiita mwenyewe mjumbe, maana wanatheolojia wote ulimwenguni wasingeweza kulielezea Hilo mbali na wewe. Lilitukia kwako! Ulikuwa pale, unajua habari Zake. Jali yale mtu mwingine ye yote asemayo, ama ni kiasi gani wanaweza kusema, "siku zimekwisha, sivyo ilivyo," wewe … ilitendeka kwako, na ni kulingana na Neno.

97 Naam, hiyo ndiyo sababu Musa alijua Sauti hii ilikuwa imenena naye, ilikuwa ni Sauti ya Neno. Alijua ya kwamba Mungu alikuwa amemwambia Ibrahimu, "Uzao wako utakuwa mgeni kwa muda wa miaka mia nne, lakini mimi nitawakomboa." Naye alijua ile miaka mia nne ilikuwa imekwisha na aliitwa kufanya hivyo.

Wanaume na wanawake, Mungu aliahidi katika siku hizi za mwisho ya kwamba angemwaga Roho Wake juu ya wote wenye mwili. Yeye aliahidi angeutuma Ubatizo wa Roho Mtakatifu, Naye angemwita Bibi-arusi asiye na doa wala kunyanzi. Yeye aliahidi kulifanya, atalifanya. Usiwasikilize hawa wachungaji wa kukodishwa, watakupoteza. Roho Mtakatifu ndiye Mchungaji wa kukulisha chakula cha kondoo kutoka kwenye Neno hili. Daima huja kwa Mchungaji. Yeye ni Mchungaji wetu. Msikilizeni, ninyi ni kondoo wa zizi Lake; kama ndivyo ulivyo, unasikia Sauti Yake. Si yale mtu mwingine asemayo, unasikia yale Yeye anayosema. Sauti ya kigeni, hujui kitu juu yake.

98 Loo, jamani, msikilizeni yule nabii-mchungaji mwenye nguvu tena, akifasiri na kuwajulisha, Yohana (wakati aliposimama katika mto Yordani), angalia yale aliyosema (alikuwa amesimama pale, akihubiri), alisema, "Saa inakuja …"

Angalia, Yohana alikuwa mwana wa kuhani. Wao daima walifuata m—mstari wa baba yao, hivyo ndivyo tulivyopata majina yetu. Kwa chochote walichofanya, waliwaita hivyo. Naye Yohana alipaswa kuwa kuhani kama baba yake.

Na, mwajua, mama huyu, alipochukua mimba, baada ya Malaika wa Bwana kukutana na babaye Zakaria, akaenda nyumbani kwa Elisabeti, naye tayari alikuwa na miezi sita katika … kuwa mjamzito. Lakini alikuwa bado hana uhai, aliogopa kwa sababu mtoto huyo hakuwa amecheza. Hilo ni jambo lisilo la kawaida.

99 Na Roho Mtakatifu, Malaika wa Bwana akamtokea Mariamu, na kumwambia ya kwamba "atapata mtoto, bila kujua mwanamume," na akamwambia kuhusu hali ya Elisabeti.

Alipanda milima ya Yuda, kumwambia Elisabeti. Na wakati alipokutana na Elisabeti, alimwambia ya kwamba yeye "atakuwa mama." Naye hangeweza kufahamu jambo hilo, "kutomjua mwanamume." Lakini yeye alisema, "Roho Mtakatifu alinitia uvuli, na kusema ya kwamba kitu hiki Kitakatifu kitakachozaliwa kwangu kitaitwa 'Mwana wa Mungu, 'nami nitamwita Jina Lake 'Yesu.'" Na mara ya kwanza ambapo jina Yesu lilipowahi kutajwa katika mdomo wa binadamu, maskini mtoto mchanga aliyekufa, katika tumbo la uzazi la mama yake, aliruka kwa furaha na kupaza sauti; na kuruka katika tumbo la uzazi la mama, na kamwe hakuwa amepokea uhai bado.

Jina la Yesu Kristo lilinena uhai ukaingia katika mtoto mchanga aliyekufa. Inapaswa kufanya nini katika kanisa linalodai kuzaliwa mara ya pili?

100 Nasi tunaketi tumechachuka kama vivimbe kwenye achali, na kuachilia mambo kama hayo yaendelee. Na unaogopa kuinuka na kushuhudia imani yako, na kulaani upuuzi huu wote, kumfanya Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele. Ni wakati wa Krismasi, ondoeni hawa akina Baba Krismasi na kadhalika, tupilieni mbali upuuzi huo wa kibiashara. Ulisikia wapi kuhusu Baba Krismasi katika Biblia? Ni hadithi za kufikirika za Kirumi, hazina maana kitu hata kidogo, hakuna kitu kama hicho. Usiwafundishe watoto wako upuuzi kama huo. Wakati siku moja itakubidi kumwambia ya kwamba yote yalikuwa ni hadithi isiyokuwa na mbele wa nyuma, basi umemdanganya mtoto wako. Na itaudhuru ushuhuda wako kuhusu Yesu Kristo, yeye atasema, "Labda ni jambo lile lile." Mrudisheni Yesu Kristo yule Nabii-Mchungaji Mkuu katika Krismasi tena ambapo ndipo mahali Pake.

101 Angalia, msikilizeni nabii huyu, Yohana, anaposimama pale. Sote tunajua ya kwamba yeye alikuwa ni nabii-mchungaji mkuu. Sasa, yeye alikuwa na ujumbe, Malaika alijua ya kwamba angemtambulisha Yesu.

Sasa, asingeweza kwenda kwenye seminari fulani. Wangesema, "Sasa, unajua ya kwamba Daktari Fulani ni mtu tu wa kuchukua mahali hapa sasa. Huna budi kumtambulisha. Nanyi mnajua ya kwamba tu …" Mnaona, asingeweza kuchanganyikana na mwanadamu.

Akiwa na umri wa miaka tisa, tunaambiwa, alienda nyikani kujiandaa mbele za Mungu. Hapo ndipo wachungaji wanapotoka. Angalia ujumbe wake haukuwa kama wa mwanatheolojia, wenye maneno makuu mno, na mazito ya digrii fulani. Yeye alisema, "Loo, enyi kizazi cha nyoka." Kumwambia mtu wa kidini, "Enyi kundi la nyoka." Hivyo ndivyo alivyokuwa ameona nyikani, alimwona yule nyoka. Kitu cha chini kabisa alichoweza kupata kilikuwa ni nyoka, naye akawaita makuhani na makasisi na wanatheolojia wa siku hiyo, "Kundi la nyoka!" Kasema, "Ni nani aliyewaonya kuikimbia ghadhabu ijayo? Msianze kusema, 'Sisi ni wa hili, na sisi ni wa lile,' kwa maana nawaambia ya kwamba Mungu anaweza kutoka katika mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto." Mawe, yale aliyokuwa ameyaona nyikani. "Pia, shoka limewekwa

kwenye shina la mti." Hayo ndiyo aliyokuwa ameona: nyoka, miti, nyika. Na, mnaona, huo ulikuwa ujumbe wake. Yeye hakujua maneno mazito mno ya daktari fulani mkuu wa kiungu (angaliweza kuyaeleza yote vinginevyo), yeye alihubiri tu kulingana na mwelekeo wa maumbile.

102 Hilo ndilo tunaloonyesha hapa: fimbo ya mchungaji, mchungaji, kondoo, mstari wa maumbile.

Alifanya nini? Alikuwa na jambo kubwa la kufanya, yeye ndiye ambaye angemjua Masihi. Akasema, "Ninasema, 'Yeye amesimama hapa miongoni mwenu sasa. Nawe humjui, kwa sababu theolojia yako imekufunga sana, hujui uko wapi.'"

Siku moja Yesu alikuja akitembea, alisema, "Tazama, yuaja Mwana-Kondoo wa Mungu aichukuaye dhambi ya ulimwengu." Mwana-Kondoo! Haleluya! Upatanisho halisi! Yule pale anakuja ambaye kila kondoo tangu Bustani ya Edeni na kuendelea ameonyesha kivuli, Mtu wa kawaida akishuka kwenda mtoni.

103 Wao walisema, "Yohana, ulijuaje jambo Hilo? Sikuona jambo moja tofauti."

"Lakini ninashuhudia, niliona Roho wa Mungu akishuka kama hua, na Sauti ikisema, 'Huyu ni Mwanangu Mpendwa Ambaye ninapendezwa kukaa ndani Yake.'"

Mwangalie Hua na Mwana-Kondoo. Mnaona? Naam. Vipi kama ingalikuwa ninii … vipi kama ingalikuwa kitu fulani … Vipi kama ingalikuwa ni mbwa mwitu amesimama pale? Vema, huyo Mwana-Kondoo asingeweza kwenda juu … ama huyo Hua … Mungu alijionyesha Mwenyewe kwa mfano wa hua, ndege aliye mpole sana kuliko ndege wote wa mbinguni; Mwanawe kwa kondoo, mnyama mpole sana kuliko wanyama wote duniani. Mnaona, ndege msafi wa mbinguni, si kunguru; si ndege mla mizoga, bali hua. Si nguruwe, bali mwana-kondoo. Maumbile mengine yo yote yasingeungana pamoja.

Na angalia wakati Hua alipokuja juu ya Mwana-Kondoo, Yeye alimwongoza. Si jinsi angefanya, bali jinsi Baba angemwongoza. Hivyo ndivyo mwana-kondoo halisi alivyo leo. Enyi kondoo wa wakati wa Krismasi, hivi hamjui ya kwamba Mungu huongoza tu kwa Neno Lake? Hiyo ni fimbo Yake.

104 Angalia hakuna kitu ambacho kingetukia, lakini Yohana alisema, "Hao wengine hawakuliona, bali ninashuhudia, 'Nililiona.'" Akiwajulisha: "Tazama, Mwana-Kondoo wa Mungu azichukuaye dhambi za ulimwengu."

Naomba sasa niutambulishe Ujumbe wangu wa Krismasi, na wakati ninapofunga sasa: "Yesu Kristo, yeye yule jana, leo, na hata milele." Ni Mwana-Kondoo yule yule. Yeye ni Mwana-Kondoo tu leo kama alivyokuwa wakati huo. Yeye yuko hapa kadiri alivyokuwa pale, kwa maana Neno Lake ni lile lile. "Walipo wawili watatu wamekusanyika katika Jina Langu, nipo hapo katikati yao." Hivyo ndivyo alivyosema hasa. Yeye habadiliki kamwe, Yeye ni Mungu Neno. Yeye habadiliki kamwe; angali anawapa kondoo Wake, na kuwalisha kwa Mchungaji-Nabii Wake, chakula cha kondoo Wake kwanza. Si kwa mwanatheolojia; kwa kondoo Wake.

105 Hawataninii … Hao wengine wanawezaje kukila. Lakini wenye hekima … Angalia jambo hili! Lakini wenye hekima na wasomi, waliofunzwa vizuri wa ulimwengu, wangali wanatamani kusema kuna Baba Krismasi. Na kuna kila namna ya uongo na upuuzi ambao wanaabudu, kwa sababu hawatamkubali, Neno; kwa sababu katika madhehebu yao, hapatani na ladha yao, wachungaji wa siku hizi. Watu walioajiriwa kutokana na kanuni za imani, ambao watataka kuwaunganisha chini ya mbuzi mmoja, msiamini! Watakuongoza machinjioni. Msikieni yule Mchungaji Mkuu aliyezaliwa miaka elfu moja mia tisa iliyopita, mwezi huu. Wakati mwingine huko ng'ambo, katika Ujumbe Wake, walikuja wachungaji wa kweli waliojua jinsi ya kuwachunga kondoo.

Ukiangalia, wangali wanatamani. Hawatakubali jambo Hilo leo, kama tu vile walivyolikataa wakati huo, kwa sababu halilingani na ladha yao ya kidini. Wanaligeuza Neno hilo na kulifanya lipatane na madhehebu yao, nao hawatahubiri Neno. Hawataweza! Wanasema, "Vema, hiyo ilikuwa ni kwa ajili ya siku za mitume. Haimaanishi jambo hili." Inamaanisha vile hasa inavyosema, haihitaji mtu ye yote ku …?… Kuwafasiria.

106 Sasa hebu katika saa hii na tuinamishe vichwa vyetu na mioyo yetu kwenye mavumbi ya nchi, na tuharakishe haraka sana kwenye hori, kuona na kupokea Nuru ambayo Neno hili huleta kwa Mchungaji: yule Nabii-Mchungaji Mkuu, Yesu Kristo Mwana ya Mungu. Nilizungumza nanyi kwa kirefu. Huenda sikuyapanga maneno yangu vizuri kama kasisi anavyopaswa kufanya, sijaribu kufanya hivyo. Ninajaribu kulinena jinsi tu anavyonipa.

Lakini, mnaona ni kwa nini ilibidi iwe ni wachungaji? Hao wengine walikuwa wamefunzwa sana katika wazo lingine hata wasingelipokea. Na leo tuna kila namna ya waangalizi, watu wa wilaya, maaskofu, makasisi, makadinali, mapapa, kila kitu ulimwenguni, kujaribu kutuongoza. Lakini Mungu alitupa Mchungaji, na Mchungaji huyo ni Roho Mtakatifu.

107 Nisikilizeni sasa. "Wakati Yeye…" (si wazo, Yeye ni kiwakilishi nafsi) "Wakati Yeye Roho Mtakatifu atakapokuja (Roho wa Kweli), atawafunulia mambo haya ambayo nimewaambia, na atawaonyesha mambo

yajayo." Huyo ni yule Mchungaji Mkuu, Huyo ndiye Mchungaji aliyeachwa na Yesu. Naye Roho Mtakatifu aliandika Biblia, Biblia ilisema hivyo, "Watu wa kale, wakiongozwa na Roho Mtakatifu, waliandika Neno." Sasa, Roho Mtakatifu angeweza kukuvuta kwenye kanuni ya imani? Je! Roho Mtakatifu angeweza kukuvuta—kukuvuta kwenye kitu ambacho Neno hili halisemi? Mbona, isingewezekana kabisa. Roho Mtakatifu angekuwa ni mwongo kama Yeye alisema ya kwamba "Hivi ndivyo mnavyopaswa kufanya," kisha ageuke na kusema, "La, lilikuwa ni kosa, basi fanyeni yale kanisa linayosema mfanye."

Sasa, kama mmekuwa mkisikiliza jambo fulani, mwingine amekuvuta akakutoa kwa Mchungaji halisi na wa kweli atakayekuongoza kwenye Neno, Roho Mtakatifu, nawe huna tukio, wala huna ushuhuda wa Roho Mtakatifu maishani mwako, ambayo bila…

108 Mungu ni Mmoja. Mungu ndiye pekee aliye na Uzima wa Milele, Naye ni Uzima wa Milele. Na chochote kilichokuwa na mwanzo kina mwisho. Na kama wewe ni mfuasi tu wa kanisa, lilikuwa na mwanzo. Lakini Neno la Mungu halina mwanzo, Mungu hana … Na wakati unapozaliwa na Mungu, umezaliwa kwa Neno, ndipo unakuwa mwana wa Mungu, na jina lako liliandikwa kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Nawe, rangi ya nywele uliyo nayo, macho ya rangi uliyo nayo, kimo ulicho nacho, Mungu alikuona kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Naye alikuona, mwanadamu, kama ulivyo wewe. Na hata ingawa miaka milioni moja ilipita, hakuna kitu cha kukuzuia kurudi kwenye ile sura kamilifu ambayo Mungu alikukusudia hapo mwanzo, "Kondoo Wangu wanaisikia Sauti Yangu, mgeni hawatamfuata."

109 Na kama hujakubali huo Uzima wa Milele, usiku wa leo, nawe unaiangalia hadithi ya u—u—uongo ya mtoto mchanga aliyelazwa ho—ho—horini, na kundi la mamajusi wamemzunguka, usiamini vitu kama hivyo. Na unajaribu kuwazia, "Vema, nitakuwa mzuri. Nami nitafanya jambo hili. Nami nitajiunga na kanisa. Na hilo ndilo tu ninalohitaji kufanya." Umepotea. Kama huna Uzima wa Milele, unawezaje kuishi milele?

Unaweza kuchukua punje ya mahindi, sijali jinsi inavyoonekana kamilifu, unaweza ku- … Sayansi imetengeneza moja, ambayo unaweza kuipasua: ina unyevu ule ule, moyo ule ule, vitu vile vile ambavyo punje ambayo imekuzwa shambani ilivyo navyo, kitu kile kile. Ungeweza kuziweka kwenye maabara, na huwezi kutofautisha moja na nyingine: moja itapika ugali mzuri tu kama hiyo nyingine, moja itatengeneza bisi zile zile. Lakini njia pekee unayoweza kuzitenganisha, ni kuzizika. Ile iliyotengenezwa na mwanadamu, inakaa mle, inaoza wala haichipuki. Lakini ile ambayo Mungu aliumba, ina chembechembe ya uhai, inaishi tena.

110 Huenda ukamwiga Mkristo, huenda ukaenda kwenye kanisa kama Mkristo, huenda ukaandika jina lako kwenye kitabu kama Mkristo, huenda ukajiunga na dhehebu kama Mkristo; hilo lingekuwa ni sawa, lakini isipokuwa huo Uzima wa Milele uwe ndani yako ambao huyo Mchungaji Mwema aliutoa kwa ajili ya Uhai Wake, kutenganisha … Wakati Mungu aliposhuka pale Pentekoste, Yeye alishuka katika mpira wa moto kama alivyofanya juu ya Mlima Sinai, kama alivyofanya kwa mchungaji wa kwanza, Musa. Na wakati aliposhuka, Yeye alijitenga Mwenyewe kwa ndimi za moto zilizoketi juu ya kila mmoja wao, Mungu akijitenga Mwenyewe katika watu Wake. Na isipokuwa umepokea kile ambacho … Petro alisema ya kwamba "Ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, kwa hao walio mbali."

111 Enyi marafiki, msisikilize hadithi yo yote ya kitheolojia, zaliweni mara ya pili. Na unapokuwa, Roho aliye ndani yako ni sehemu ya Mungu, na anashuhudia kwa kila Neno la Mungu kuwa "Kweli." Kama huna ujuzi huo, hebu sasa tuharakishe kwenda kwenye hori, Neno. Hebu na tuharakishe kwenye Biblia, mbali na haya makanisa yaliyopambwa ya kitheolojia, kwenye hori halisi, kwenye Neno la Mungu ambapo Masihi anajulikana.

Huku vichwa vyetu vimeinamishwa, hebu na tuombe.

112 Mungu mpenzi, hayo tu ndiyo ninayojua kusema wakati huu. Tunakaribia Krismasi, barabara zimejaa wanaume na wanawake, wavulana na wasichana, wakisukumana, wakiburuzana, wakijaribu kununua zawadi kumrudishia mtu ambaye angewapa vivyo hivyo. Watu wengi wanaojiita Wakristo wako nje mitaani wakinunua sigara, pombe, kwa ajili ya zawadi za Krismasi. Mungu, inaonekana kana kwamba wanaitupa moja kwa moja usoni Mwako, wakiwafundisha watoto wao hadithi za uongo, theolojia ya Kirumi na kikafiri ya Mtakatifu Nicholas, kisasili fulani ambacho kinakubalika kwa urahisi na ulimwengu, nao wanamkataa Kristo halisi wa Krismasi, Mwana-Kondoo halisi.

Mungu, naomba, usiku wa leo, ya kwamba tunapovielekeza vichwa vyetu kuelekea mavumbi uliyotutoa kwayo, … Ulimwambia Ibrahimu wakati mmoja, yule nabii-mchungaji mkuu, "Nenda zako, Ibrahimu, ukahesabu mchanga ulio pwani ya bahari."

Naye akarudisha neno, "Hauhesabiki, siwezi kuuhesabu."

Ndipo ukasema, "Angalia juu mbinguni, na uzihesabu nyota." Naye alijua ya kwamba hilo halingewezekana. Nawe ukamwambia, "Ndivyo utakavyokuwa uzao wako." Tunaangalia ujumbe huo kwa

huyo nabii-mchungaji, "kutoka kwenye mavumbi ya nchi, hadi kwenye nyota za mbinguni," ya kwamba ingawa kuna mauti katika miili yetu inayopatikana na mauti ya kutupeleka mavumbini, kuna Uzima unaoweza kutuinua hadi kwenye nyota.

113 Kama vile ulivyomwambia nabii Wako mkuu Danieli, "Na hao wamjuao Mungu wao, katika siku za mwisho, watatenda mambo makuu. Na hao waongozao wengi kutenda haki watang'aa kuliko nyota milele na milele."

Bwana Mungu, Muumba Mkuu, Ambaye alikuwa tayari kuja duniani katika umbo la Yesu, kumfanya mwanadamu ajue Mungu alikuwa nini. Nawe ulikuwa Wewe pekee uliyeweza kuchukua adhabu ya mauti, hakuna Malaika, hakuna kibadala angeweza kufanya hivyo. Wewe Ndiye uliyeweka adhabu, na Wewe peke Yako ungeweza kuiondoa. Na ukiwa Roho, usingeweza kufa. Lakini ulifanyika mwili kusudi upate kufa; na uwe Mwana-Kondoo upate kuondoa dhambi ya Wale Uliowakomboa, ambao ilikubidi kuwakomboa kwa Damu Yako Mwenyewe.

Loo, hadithi hiyo ni kuu sana, Bwana, inapita juu ya vichwa vya watu wengi sana. Kuwaza: "Yehova mdogo, akiwa amelala katika hori, ilimbidi kuishi kama mtoto mchanga. Maskini Yehova, alizaliwa katika zizi. Maskini Yehova, akicheza na watoto barabarani. Maskini Yehova, yule kijana. Maskini Yehova, yule mvulana wa shule. Na Yehova, Mwenye Nguvu." Ulichukua mahali hapa pote. "Na halafu, Yehova, Mwana-Kondoo. Yehova, Nabii." Nawe ukawa haya yote upate kupata adhabu ya dhambi, na kutupa Uzima wa Milele.

114 Tusamehe, Ee Mungu, sisi, maskini, viumbe visivyostahili vya ulimwengu huu. Tunafedheheshwa usiku wa leo, Bwana, tunaposoma yale uliyotufanyia, na ni madogo sana tuliyoyatenda. Jinsi ulivyokuja katika siku za viongozi wakuu wa dini! Jinsi ulivyokuwa tayari kusimama na kuliakisi Neno la Baba! Jinsi ambavyo Hukupatana juu ya nadharia zao! Na leo inaonekana kana kwamba hakuna mtu anayetaka kusimama na kuita Neno kwamba lingali ni "Neno," na pasipo kupatana. Tunaomba, Mungu, utusamehe kwa ajili ya mambo haya ambayo tumeyapuuza sana. Na utupe usiku wa leo, mioyoni mwetu, tunapokupa Wewe kama hori. Nasi tunajua ya kwamba kila wakati ambapo Kristo aliyesulubishwa anakubalika, kuna kuzaliwa upya, kuna kondoo aliyezaliwa upya, kuna kuimba Mbinguni kwa Malaika. Juu ya mwenye dhambi mmoja anayetubu, Malaika wanaimba tena.

Tunaomba, Mungu, ya kwamba kama kuna wengine hapa usiku wa leo wasiokujua Wewe kama Karama halisi ya Mungu, kama Mwokozi binafsi, si kwa mawazo tu ya akili, bali kwa kuzaliwa upya (kwa kuzaliwa na Roho Wako) , jalia wapokee sasa hivi, Bwana, huku vichwa vyetu vimeinamishwa. Na kama kukiwepo na mmoja, Bwana, ambaye hajafanya jambo hili, jalia mioyo yao ipokee furaha sasa, na wapate kama wachungaji wa kale, katika hori la moyo wao, Neno, Masihi; hilo litathibitishwa kwao kama Roho Mtakatifu, Mchungaji Mkuu wa siku hizi. Tunaomba hili katika Jina la Yesu.

115 Wakati tukiwa tumeinamisha vichwa vyetu, nami natumaini mioyo yetu imeinamishwa, je—ungeomba, ndugu yangu mpendwa, ingawa wewe ni mfuasi wa kanisa … Nami ninatumaini ya kwamba sijawaudhi kwa kusema yale niliyosema. Mimi … Ni sawa kuwa mfuasi wa kanisa, tunapaswa kufanya hivyo, lakini, Ee ndugu, usikubali tu jambo hilo, huna budi kuzaliwa mara ya pili. Hivyo ndivyo yule Nabii-Mchungaji Mkuu alivyosema, "Hamna budi kuzaliwa mara ya pili." Yeye alisema hayo kwa mwanatheolojia, "Huna budi kuzaliwa mara ya pili."

Na wakati unapozaliwa mara ya pili, si kwa sababu tu unaamini. Wanasema, "Unazaliwa unapoamini."

Lakini Biblia ilisema, "Ibilisi anaamini, pia." Sasa, angalia, si hivyo, ni tukio.

Unasema, "Vema, nimeishi maisha mazuri."

Vivyo hivyo na mitume, bali hawakuzaliwa mara ya pili mpaka walipompokea Roho Mtakatifu. Hata hawakuwa wameongoka mpaka walipompokea Roho Mtakatifu. Mnakumbuka ule usiku kabla ya usaliti … ama juu ya usaliti, kabla tu ya usaliti huo kutukia? Yesu alimwambia Simoni Petro, "Utakapoongoka, waimarishe ndugu zako." Naye Petro alikuwa amemfuata kwa muda wa miaka mitatu na nusu, na alikuwa ametoa pepo, na kuwaponya wagonjwa, alikuwa amehubiri Injili, na hata hivyo (kulingana na Neno) hata hakuongoka.

116 Sasa, ungetaka aina hiyo ya—ya Mjumbe moyoni mwako usiku wa leo? Kama—kama kweli unataka Hilo … Haileti tofauti yoyote yale mtu mwingine asemayo, ni kweli, ndugu, dada. Ninajua hilo ni kweli. Ungeweza, wakati kila kichwa kimeinamishwa na kila jicho limefumbwa, si kwangu mimi, mimi ni mwanadamu tu, ndugu yako, lakini kwa Kristo ungeinua mkono wako, useme, "Ninaamini Hilo. Nami kweli ninataka huyo Kristo aingie moyoni mwangu, Kristo halisi wa Krismasi"? Waweza kuinua mkono wako sasa? Mungu akubariki. Hilo ni zuri. Mungu akubariki, pia. Mungu akubariki. Jamani, mikono kila mahali.

Hebu litukie, ndugu; hebu litukie, dada; hebu litukie, rafiki yangu; mjazwe na Roho wa Mungu. Inaleta tofauti gani yale mtu mwingine ye yote asemayo? Kumbuka, ni maisha yako. Huenda hata tusiwe duniani asubuhi, hatuna—hatuna hakikisho la uhai zaidi ya vile tulivyo na pumzi puani mwetu sasa.

Huenda tusipate pumzi nyingine, ila neema ya Mungu. Na linafaa nini, haidhuru umeishi vizuri jinsi gani na nini …? Yesu alisema, "Mtu asipozaliwa mara ya pili, hataingia kamwe."

117 Sasa, ninajua istilahi za kuzaliwa mara ya pili ni nini, lakini hebu na tuangalie tu yale yaliyotukia katika Biblia walipozaliwa mara ya pili. Petro alikuwa mwamini, mitume walikuwa waamini, bali hawakuzaliwa mara ya pili mpaka baada ya Roho Mtakatifu kuwashukia Pentekoste. Sasa, walikuwa wakishangaa kilichotukia, na Petro akasema, pamoja na hao wengine, "Enyi watu wa Israeli, lijulikeni jambo hili; Yesu wa Nazareti, mtu aliyethibitishwa na Mungu miongoni mwenu kwa ishara na miujiza na maajabu, aliyofanya Mungu kwa kwa mkono Wake; Yeye aliyejulikana tangu zamani, kwa halmashauri iliyoamuliwa mlimchukua kwa mikono ya waovu na kumsulubisha, ambaye Mungu amemfufua nasi tu mashahidi Wake. Yeye amekimwaga kitu hiki mnachokiona na kukisikia sasa, na ni kulingana na Maandiko."

Ndipo basi, waliposikia jambo hili, walichomwa moyoni mwao, na kusema, "Waume na ndugu zetu, tufanye nini tupate kuokolewa?"

Petro akawaambia, "Tubuni!"

118 Sasa, rafiki yangu Mkatoliki anayeketi hapa, ambaye ninawajua wanne ama watano wenu mnaoketi hapa. Nilikuwa nikizungumza jambo hili na kasisi wenu, labda si kasisi wenu, bali mmoja wa makasisi wa Kikatoliki, yeye alisema, "Yesu alilipa kanisa nguvu za kuondoa dhambi, 'Wowote mtakaowaondolea dhambi, wameondolewa; wowote mtakaowafungia dhambi, zimefungiwa.'" Hiyo ni kweli. Lakini hebu tuangalie jinsi alivyofanya jambo hilo, jinsi mitume walivyofuata agizo Lake, si kulingana na jinsi ambavyo —ambavyo kuhani anafanya leo.

Lakini kasisi wa kwanza, kama unataka kumwita hivyo, Petro, ambaye alikuwa na funguo za Ufalme, alisema lifanyweje? Yeye alisema, "Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina Lake Yesu Kristo mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa maana ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa hao walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie." Na kama Mungu angali anaita, tukio lile lile ni kwa ajili yako kama utafuata maagizo yale yale. Kama kusanyiko hili linaamini Hilo, huku vichwa vyenu vimeinamishwa, semeni, "Amina." [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Basi, chochote pungufu ya Hilo ni kinyume cha Neno, wala si kulingana na Mchungaji.

119 Bwana Yesu, wako mikononi Mwako sasa. Ninaomba ya kwamba kila moyo uliofunguliwa usiku wa leo ambao hauna Kristo, Masihi (na Kristo ni Neno, Neno lililotiwa mafuta likidhihirishwa), na kukiwapo mioyo yoyote iliyofunguliwa hapa usiku wa leo ambayo haina Masihi huyo (ile Karama halisi ya Krismasi, Karama pekee halisi ya Krismasi iliyopo, ambayo Mungu aliupa ulimwengu, na kuitangaza kwa ulimwengu kwa wachungaji, wa Kondoo Wake, ule Upatanisho kwa ajili ya dhambi), na kama moyo huo umefunguliwa usiku wa leo, uweke ndani yake, Bwana, Neno Masihi la siku hizi. Tunawakabidhi Kwako katika Jina la Yesu Kristo, Mwanao. Amina.

120 Je! Mnampenda? Mnamwamini? "Utafuteni kwanza Ufalme wa Mungu, na haki Yake, mambo mengine yote mtaongezewa."

Marafiki, kabla hatujaachana, ninataka kusema jambo hili. Mara nyingi, ninaeleweka vibaya sana. Nina Ujumbe kutoka kwa Mungu, nami sina budi kutangaza Ujumbe huo bila kujali. Ninajua unaeleweka vibaya. Kama haukueleweka vibaya, basi usingekuwa ni Ujumbe wa Mungu; usingeweza kuwa. Kuna vurugu nyingi sana hivi kwamba usingeweza kueleweka. Ninaamini ya kwamba Mungu ana mwanadamu katika kila dhehebu na shirika la ulimwengu, na si kwamba mimi ninawapinga ndugu zangu. Nilikuja hapa Tucson, miaka mitatu iliyopita, nami nilifanya mkutano pamoja nanyi wahudumu huko kwa Ndugu Gilmore, na iliulizwa, je! nilikuja "hapa kuanzisha kanisa?"

Nikasema, "La, bwana. Nimekuja hapa kukusaidia." Lakini sijaulizwa bado, katika miaka mitatu. Lakini vivyo hivyo, niko hapa kuwasaidia. Nipo hapa kushikana mikono pamoja nanyi, si kujiunga na madhehebu pamoja nanyi, bali kushikana mikono na moyo pamoja nanyi kwenye Neno la Mungu, kujaribu kuihubiri Injili kwa kila nafsi iliyopotea na kila mtu mwenye haja ambaye yuko kwenye masafa ya sauti zetu.

Ninajitolea kwa Mungu, usiku wa leo, kwa moyo wangu wote, kwa yote yaliyo ndani yangu. Sina mengi sana ya kutoa; Siwezi kuleta uvumba, manemane, na dhahabu, maana sina kitu. Lakini yote niliyo nayo ndani yangu ambayo Mungu alinipa, maisha haya, ninayaweka wakfu Kwake upya usiku wa leo, juu ya hori la Neno Lake moyoni mwangu; na kumwahidi, kusimama na Neno hilo, kama ataniruhusu kuishi mwaka mwingine, kwa uaminifu tu niwezavyo kusimama; kuhubiri kila kipengee Chake, na kuamini kila sehemu Yake; kwa hiyo, nisaidie, Mungu. Je! Mtafanya vivyo hivyo pamoja nami?

121 Tupokee, Bwana. Tunapokea Karama Yako ya Krismasi, Masihi, Neno lililotiwa mafuta linalothibitisha Uwepo Wako pamoja nasi, Bwana, bila kujali kanuni za imani ama madhehebu. Tunaona, sisi wenyewe leo, ulimwengu ukisambaratika, na huyu hapa yule Masihi mkuu amesimama huku ameinyosha mikono Yake: Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele, aliyetoa ahadi hizo, ya kwamba katika siku hizi za

mwisho, kanisa lingeunda madhehebu sana mpaka lingeingia katika Laodikia. Nasi tunaona jambo hilo leo, Bwana.

Tunaweza kufanya nini, Mungu mpendwa? Nifanye nini? Nisaidie mimi na hawa wachungaji wengine, Bwana, kote ulimwenguni, wachungaji wa Neno, kulitangaza, Bwana, katika mwaka huu ujao. Tusaidie, Bwana, tunaomba. Tupe Upendo Wako na Roho Wako na Nuru Yako. Tunajiweka wakfu usiku wa leo kwa Neno Lako na kwa wito Wako. Katika Jina la Yesu Kristo, tunapokea Karama Yako ya Krismasi: Neno la Mungu lililofanyika mwili ndani yetu. Amina.

122 Ninapenda nyimbo za kanisa. Paulo alisema, katika Biblia, "Nilipoimba, niliimba katika Roho. Ninahubiri, ninahubiri katika Roho. Wakati mimi … lo lote ninalofanya, ninafanya yote katika Jina la Yesu Kristo." Sasa, kwa kuwa Hili limekuwa gumu juu yenu … Nami na—nawapenda. Ninakuja na Ujumbe huu. Wakati mwingine inaonekana kana kwamba ninachukia tu kulisema, lakini hata hivyo nina—nina wajibu, ndugu. Nisipofanya hivyo, mimi ni mnafiki. Nisipofanya hivyo, mimi ni msaliti kwa dhamiri yangu mwenyewe, na imani yangu—yangu mwenyewe katika Neno la Mungu. Sina budi kufanya hivyo, si kuwa tofauti, bali kuwa mwaminifu kwa wito wangu. Nami nataka kuwasaidia nyote, ninataka kufanya kila niwezalo.

Sasa hebu na tuimbe moja ya nyimbo kuu za nyakati zote, naupenda sana, Nampenda. Mnajua, ninaamini kama sote tungempenda tu, tungefanya yale aliyotuagiza kufanya. "Mnaniitaje Mimi, 'Bwana,' wala hamfanyi mambo ninayowaamuru kufanya? Mnaniitaje, 'Bwana,' halafu msifanye yale niliyowaambia kufanya?"

123 Ama ungetaka kumsikiliza mchungaji wa mshahara ambaye angesema "weka jina lako kwenye kitabu, na ujiunge; kula ushirika huu, useme hivi, na ndivyo inavyotakiwa," wakati yule Mchungaji Mkuu Mwenyewe alisema "mtu asipozaliwa mara ya pili hawezi hata kuuona Ufalme wa Mbinguni"?

Na waangalie hao wanatheolojia waliofunzwa wa siku hiyo, waliofunzwa! Mtakatifu? Maisha safi? Hatuna kitu cha kuwalinganisha nacho leo, jinsi walivyoishi. Na yule Mchungaji Mkuu aliwaita nini? Kasema, "Ninyi ni wa baba yenu Ibilisi," kwa sababu hawakuninii … Walilitambua Neno, bali Neno la siku nyingine, si Neno la siku hiyo.

Kama walitambua wakati wa Nuhu, hiyo ni sawa, huo ulikuwa wakati wa Nuhu; bali halingefaa katika wakati wa Musa. Na wakati wa Musa haungefaa kitu katika wakati wa Kristo. Mnaona? Wakati wa Luther hautafaa kitu katika wakati wa Wesley. Wakati wa Wesley hautafaa kitu katika wakati wa Pentekoste. Na Wapentekoste wamefanya jambo lile lile wengine wao walifanya. Sasa, ni nani aliyenisaidia katika siku zilizopita? Niliwauliza.

124 Wakati majani ya nyasi yanapotokea, ni kitu gani? Nini … wakati jani la ngano linapotokea. Yesu alisema, "Mbegu ya ngano isipoanguka ardhini." Inakuwaje wakati punje ya ngano … ama ngano ikianguka ardhini? Jambo la kwanza linalojitokeza ni jani dogo. Ni—si kama punje iliyoingia. Angalia maumbile. Si kama ile punje iliyoingia, bali ni mbebaji wa Uhai wa punje. Kilichotokea …

Yule kafiri ambaye ndiyo kwanza aandike kile kitabu kinachojulikana sana, *Mungu Mkimya*, kilisema, "Kunawezaje kuwako na Mungu ambaye angeweza kuifungua Bahari ya Shamu, na kusimama na kuvumilia miaka elfu moja ya nyakati za giza na kuwaona watoto wadogo wakiliwa na simba, na watu wakitundikwa misalabani, na kuuawa kinyama kwenye viwanja vya michezo na kadhalika, wala hata asifungue kinywa Chake?" Mnaona, Neno ni ufunuo.

125 Hiyo ngano, wakati hiyo ngano halisi ilipoanza hapo mwanzo, ilishindwa mbele za Mungu. Na hatimaye kukaja Ngano fulani, muakisi halisi wa Mungu, ambaye aliakisi Neno Lake lote hivi kwamba hata Yeye alikuwa ni Neno. Ndipo Mungu akampa Bibi-arusi kwenye Pentekoste; bali yule Bibi-arusi alianguka ardhini katika nyakati za giza, kama tu vile ngano halisi ilivyofanya, Ilianguka ardhini. Na kwa nini isingeweza kutenda kazi? Kwa sababu ilikuwa imefichwa chini ya nchi, ilibidi ioze kabla haijaweza kuleta uhai.

Lakini alikuja maskini kasisi mdogo wakati mmoja, jina lake Martin Luther, naye akachipusha lile Neno moja la Kweli: "Wenye haki wataishi kwa imani," kukatokea unyasi; kisha unyasi mwingine ukafuata huo, Zwingli, ndipo akaja Calvin na Knox na kuendelea.

Jambo la kwanza unajua, ilibadilisha jani lake, ikaingia kwenye kishada. Sasa, hicho kilionekana kidogo kinafanana zaidi nayo, bali kingali hakikuwa kile kitu halisi kilichoingia ardhini, Wesley akafuata moja kwa moja. Kutoka kwa Wesley kulitokea kanisa la Kimethodisti, kutoka kanisa la Kimethodisti kukaja Wanazarayo, Umoja wa Ndugu, na kadhalika. Ilifanya nini? Ilianguka tena na ikazaa, ilionekana kama punje halisi ya ngano sasa, Pentekoste.

126 Sasa, mwangalie Yesu, katika Mathayo 24:24, "Katika siku ya mwisho, hizo roho mbili zitakuwa pamoja sana hata zitawadanganya walio Wateule, kama yamkini." Sasa, wakati punje hiyo ya ngano ilipotokea, mkulima yeyote wa ngano anajua ya kwamba hiyo ilionekana kama kamilifu, punje ya ngano. Lakini wewe keti chini na kuichukua mkononi mwako, ifungue. Hamna ngano ndani yake, ni kapi. Lakini huko nyuma kabisa, chini ya darubini unaweza kuona chipukizi dogo sana, hiyo hapo punje inakuja.

Halafu basi hilo kapi lifanye nini? Ni kulinda nafaka, jua kali lingeiua, linalinda punje mpaka punje imekomaa. Na halafu wakati punje inapokomaa, kapi linajiondoa kwake. Lakini, je! Mliona, hiyo punje basi inayokuja, haina budi kuwa ni punje ya aina ile ile iliyoingia ardhini.

127 Baada ya ufufuo wa Luther, lilikuja dhehebu. Baada ya ufufuo wa Wesley, likaja dhehebu. Baada ya Alexander Smith, Yohana … Alexander Campbell, John Smith, hao wengine wote, kukatoka dhehebu. Baada ya Pentekoste, moja kwa moja kama jambo halisi, bali lilikuja dhehebu. Ilifanya nini? Lilijiondoa.

Tumekuwa na miaka kumi na mitano ya uamsho, haijapata kujulikana katika historia yote. Na angalia, katika ufufuo huu wa miaka kumi na mitano, unaenea kote ulimwenguni, na hakuna dhehebu hata moja limejengwa kutoka Kwake. Ulikuwa wapi? (Ulianzisha mvua ya vuli, ukafa katika ninii yake…mara moja, ulikufa.) Kumekuwa hakuna dhehebu linalofuata Hili. Kwa nini? Ni punje Yenyewe, hakuwezi kuwako na nyingine. Na kapi sasa linajiondoa, hakuna ushirikiano, hakuna mtu anayekutaka. Kwa nini? Haina budi kuwa Hiyo.

128 Kwa nini kanisa hilo liliwekwa pale? Kuliunga mkono. Ambapo … Ni nani angaliweza kushirikiana? Ni Mbaptisti gani, ama Mpresbiteri, ama Mlutheri angeweza kuunga mkono uamsho wa uponyaji wa Kiungu? Sasa wakati Kweli inapotokea, ni kitu gani kinachotukia? Si kapi; bali Uhai unatoka moja kwa moja kutoka kwenye kapi, unaingia moja kwa moja kwenye punje, Uhai halisi wa kweli. Dhehebu linasimama pale, linakufa, kama tu vile limefanya katika kila wakati, linafanya vile vile. Mlitoka katika jambo hilo, miaka hamsini iliyopita, na mkarudi moja kwa moja tena! Lakini Maisha halisi yanafuata punje, tuko katika wakati wa mwisho, ndugu.

129 Kwa nini ikajiondoa? Kusudi ipate kuleta hiyo punje uweponi pa Mwana, ipate kuivisha hiyo punje kwa mwivisho wa dhahabu kwa ajili ya Bwana. Kwa nini imeondoka? Kwa hiyo, inasababisha maumivu ya moyo, machozi, kwamba hawajianiki mbele ya j-u-a, bali M-w-a-n-a, wapate kuivishwa waifikie Injili kamili ya kweli, wapate kudhihirisha kila kitu ambacho Yesu Kristo aliahidi katika Biblia. Kunainuka Mwili fulani leo miongoni mwa watu. Wala hakutakuwako tena na madhehebu zaidi, yanaenda moja kwa moja yanaingia katika Laodikia tajiri. Madhehebu yamefanikiwa kwa nini? Mamilioni ya dola, na mamilioni ya watu.

Na huyo Mchungaji alitoka wapi? Kuwakomboa ndugu Zake kutoka utumwani. Si—sijui; Mungu, kuwa pamoja nasi, tusaidie. Someni Neno! Yachunguzeni Maandiko! Ndani yao tunafikiri tuna Uzima wa Milele, na hao ndio wanaoshuhudia Kweli. Mnaona, Mungu aliweka Maneno Yake kwa kila wakati. Wakati huu daima …

130 Yesu alisema nini alipokuja? Yeye aliwaambia watu hao, "Enyi wanafiki! Mnazipaka kuta rangi, na kujenga makaburi ya manabii, na baba zenu ndio waliowaweka mle ndani. Nanyi ni wana wa baba zenu. Na kazi walizofanya, wewe pia utazifanya." Daima inabaki vile vile, ndugu zangu.

Lakini wakati Yesu atakapokuja siku moja, yule Mchungaji Mkuu wa kondoo kutoka kwa Pentekoste kupitia kwa Luther kupitia nyakati zote, wale ambao wamekubali Nuru jinsi ilivyokuja kupitia kwa wabebaji (si walikubali bebaji, waliikubali hiyo Nuru; mnaona, wakatoka), Yeye atakuja kuwakomboa. Nina furaha sana kwamba ninajua Yeye yuaja tena. Loo, ungehesabiwa pamoja na kundi Lake? Ungehesabiwa? Kuna njia moja tu ya kufanya jambo hilo, si kwa kujiunga na kanisa, bali kwa kuzaliwa ndani Yake. "Na wote alionipa Baba, watakuja Kwangu, wala hakuna mtu awezaye kuja isipokuwa Baba Yangu amwite." Mnaona, ni hilo lote tu ndiyo, likubali Hilo. Yeye … Hiyo ndiyo Karama ya pekee ya Krismasi ninayoijua, ni karama ya Mungu ambayo aliupa ulimwengu, Mwanawe wa pekee. Naye ni yeye yule, jana, leo, na hata milele, Neno. Mnaona? Mwamini Yeye katika siku hii, utimilifu wa Biblia.

131 Wakati hizo siri saba … Huko nyuma kupitia zile Nyakati Saba za Kanisa, kulikuwa na siri saba zilizofichwa. Ninaandika kitabu Chake. Na mwanatheolojia mashuhuri akaniambia si muda mrefu uliopita, kasema, "Ndugu Branham …" Mnaona jinsi Shetani atakavyojaribu kukuondoa njiani? Akasema, "Ndugu Branham, unajua nini? Ninaamini Bwana atawafunulia yale tutakayofanya baadaye. Ni kuninii … itakuwa siri fulani kuu iliyofichwa chini ya Mihuri hii Saba."

Nikasema, "La, hilo silo, ndugu."

Yeye alisema, "Litakuwa ni jambo ambalo hata halijaandikwa katika Neno."

Nikasema, "La! La! Unasahau, 'Ye yote atakayeongeza neno moja, ama kuondoa Neno moja.'" Mnaona, tayari liko mle ndani, lakini watengenezaji wameshindwa kuliona, hawakuishi muda mrefu vya kutosha kuliona.

Na nyakati zimekwisha sasa, tuko papa hapa Laodikia. Na kumbukeni, wakati wa Laodikia, Yeye alikuwa nje ya kanisa, akibisha, akijaribu kurudi ndani: Hawa alikuwa amemtoa Adamu wake. Mungu, tusaidie. Hebu na twende nje ya kambi kumpata. Jalia tuteseke nje ya malango pamoja Naye. Hebu na tumwendee Yeye katika mauti Yake, katika kuzikwa Kwake, na katika kufufuka Kwake; kwa kuwa ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

132 Hebu na tuimbe wimbo mmoja kabla hatujaondoka. Sivyo? Nampenda. Waweza kutupa sauti yake, dada? Ni wangapi wanaojua ule wimbo wa kale? Mimi … Kama umewahi kuwepo kwenye mikutano, ninaupenda.

Sasa hebu na tufunge tu macho yetu, tumfikirie Yehova. Hakuna mtu aliyestahili, hakuna mtu angeweza kufanya hivyo ila Yeye. Naye akashuka, akawa mtoto mchanga. Yeye alikuja, kijana. Yeye akawa seremala, mtu anayefanya kazi. Alifanyika Mwana-Kondoo, akawa dhabihu. Yeye alifufuka kwa ushindi, Yehova. Na kama vile Musa alivyoutoa mkono wake kutoka kifuani mwake juu ya moyo wake, Mungu aliutoa mkono Wake kutoka kifuani Mwake (siri Yake) Mwanawe aliyepigwa na ugonjwa wa dhambi, isiyotibika; kisha akaurudisha kifuani tena, na kuutoa na kuuweka kwako na kwangu mimi: "Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele."

Mwangalie sasa.

Nampenda, nampenda
Kwa sababu Yeye alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Kwenye mti wa Kalvari.

133 Ni wangapi wanaojua ilibidi iwe ni mchungaji, sema "Amina." [Kusanyiko linasema, "Amina."- Mh.] Lazima! Kwa nini mchungaji? Ilibidi iwe hivyo. Sasa wakati tunapoimba aya hii hii tena, nyosha mkono mezani. Kuna Wamethodisti, Wabatisti, Waluteri, Wapresbiteri, Wakatoliki, na wote, wanaoketi hapa usiku wa leo. Peaneni mikono, useme, "Msafiri mwenzangu, nina furaha sana kuwa hapa pamoja nawe, usiku wa leo." Waambie jambo fulani. Semeni, "Mungu awabariki," tunapopeana mikono sisi kwa sisi sasa. Tunapouimba tena sasa.

Mimi …
[Sehemu tupu kwenye kanda — Mh.]
… Wokovu wangu
Mtini pa Kalvari.

Sasa hebu na tufunge macho yetu na kuinua mikono yetu, na kumwimbia.

Nakupenda, nakupenda
Sababu Yeye alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini pa Kalvari.

134 Na sasa, Mungu hana umbo. Kwa hiyo, hebu na tuinamishe vichwa vyetu na kuuvumisha sasa, kama watoto wadogo, ninyi ni watoto wa Mungu. Usiangalie kile ulimwengu unachoweza kuwazia, unaabudu sasa, ukimwabudu Kristo. Inamisheni tu vichwa vyenu na kuvuumisha. [Ndugu Branham na kusanyiko wanavumisha nampenda — Mh.]

Hivi hujisikii kama uliesuguliwa kabisa? Ni kama tu … kitu fulani kimeondoa shaka yote na ulimwengu mbali na wewe? Unajisikia hivyo? Inueni mikono yenu, "Ninajisikia tu niliesuguliwa kabisa. Ninajisikia tofauti. Ninajisikia kama nimekuwa nikila kutoka mikononi Mwake. Nina, …" Kama vile ndugu hapa alivyoshuhudia, "Chakula, chakula cha Mchungaji, chakula cha kondoo." Hilo ni Neno.

135 Kondoo wa Mungu hula Chakula Chake, "Mtu hataishi kwa mkate tu, bali kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu." Na hili ndilo Hilo, Biblia. Tunakula kila Neno, si baadhi tu ya Maneno, bali kila Neno linalotoka. Loo, hilo halikufanyi umpende? Kufikiri ya kwamba sasa tuna Uzima wa Milele! Si kwamba tutakuwa, sasa sisi ni wana wa Mungu. Si kwamba tutakuwa, sasa! Na ni kuketi pamoja katika ulimwengu wa roho katika Kristo Yesu. Na ile televisheni kuu, ambayo hutangaza kuna mawimbi ya anga za juu yanayowafanya watu (mtu anayezunguka dunia) watambulikane kwa—kwa skrini ya televisheni. Neno kuu la Mungu, na Roho wa Mungu akichukua Neno la Mungu, humwakisi Yesu Kristo katika ulimwengu wa roho kwa kondoo Wake, ya kwamba ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Yeye si ni wa ajabu? Waajabu! Mungu akubariki.

136 Sasa hebu na tusimame kwa muda kidogo. Mna mtu wa kuomba baraka? Sasa, kumbukeni, wakati wa Krismasi, mwabuduni Bwana Yesu. Mwabudu katika Nguvu za kufufuka Kwake. Na kama ninaweza kuwa mwenye neema kwako (wewe, mchungaji wako, kanisa lako, ama cho chote kile), usiku kamwe huwa giza sana, mvua hainyeshi kwa nguvu sana.

Hivi majuzi usiku (kuna mama anayesimama hapa sasa) nilikuwa na shughuli nyingi sana, niliwachukua wagonjwa na kadhalika mpaka… Kulikuwa na mwanamke mwenye umri wa miaka themanini na kitu ambaye alikuwa amerukwa na akili, naye alikuwa … aliwazia kuhusu kupata mtoto ama kitu fulani, alikuwa amerukwa na akili. Naye Billy, kutoka ofisini, akanipigia simu, akasema, "Baba, unaweza?"

Nikasema, "Siwezi sasa hivi. Kuna watu … Siwezi kufanya hivyo."

Akasema, "Baba, unaweza kwenda kwenye maombi? Nitawaambia unaomba."

Nikasema, "Naam." Na wakati huo huo akajirudia. Akalala usingizi, akaamka akiwa katika hali yake ya kawaida; akala chakula kizima cha jioni cha kuku, akiwa na akili timamu. Mtu alikuwa amesimama hapa akishuhudia jambo hilo muda mchache uliopita.

137 Ndugu Mack, nilimwona hapa muda mfupi uliopita, mahali fulani kanisani. Yeye yuko hapa, mmoja wa wachungaji, mchungaji wa mahali hapa. Ndugu mpendwa sana, nami daima nimempenda Ndugu Mack tangu nilipoanza huduma. Na ndipo nikakutana naye …

Nami nilikuwa huko juu British Columbia; na kukuonyesha tu jinsi ambavyo Mungu atatenda kila kitu sawasawa. Nilikuwa tayari nimepanda farasi, na nilikuwa nikirudi nyikani ambako nilikuwa nimeongoza kundi zima la Wahindi kwa Mungu; nao wote walikuwa wameongoka, na walikuwa wamempokea Yesu.

Na kwa unabii uliomwambia yule mvulana wa Kihindi aliyepoteza farasi wake, miaka miwili iliyopita, alimwambia mahali angeupata, umbali gani angekuwa, na mahali ambapo farasi huyo angekuwa amesimama. Mama yake akifa kwa ugonjwa wa moyo. Aliponywa na kuokolewa. Na mvulana huyu, akipitia tu na kuona jambo hilo, na akijua ya kwamba yeye … farasi wake alipatikana jinsi hasa alivyoambiwa, na kila kitu.

138 Hakuna Neno hata moja ambalo Bwana amewahi kunena … Nitamwuliza yeyote wenu, "Je! Yeye… umewahi kumsikia akisema lolote, ambalo amepata kuniambia niwaambie, ila lile lililotimia vivyo hivyo hasa?" Kama hiyo ni kweli, semeni "Amina." [Kusanyiko linasema, "Amina."- Mh.] Mnaona? Mnaona? Hakika, kamwe haijashindwa hata wakati mmoja.

Na Ndugu Mack alikuwa amelala mahututi, na ikawa kwamba mke wake alimwita Billy … mke wa mwanangu, na kumwambia … aliuliza nilikuwa wapi; maskini bibi huyo mzuri na … mkewe. Naye … Na binti mkwe wangu akasema, "Yuko huko kaskazini mwa British Columbia kwenye ziara ya kuwinda."

Na asubuhi hiyo, kwa namna fulani, si—si—singempanda farasi huyo nje. Ndipo Billy akasema, "Nitaamini nitapiga simu nyumbani tena." Naye akapanda kwenye nguzo kupiga simu. Na hawa hapa wanarudi mbio, wakati maskini yule Mhindi amesimama pale, yule … yule aliyekuwa na farasi mdogo, na kusema, "Ndugu Mack yuko mahututi, naye anakuita."

139 Nami nikatoka, nikaenda mwituni na kupiga magoti. Nikasema, "Mungu mpenzi, huko chini kabisa, maili elfu tatu kote nchini, katika jimbo lenye jua la Arizona, huko Tucson, ni ndugu yangu, naye yuko mahututi. Utamsaidia?"

Kitu Fulani tu kiliniambia, "Yote ni shwari."

Na nilipomjia Ndugu Mack hivi majuzi, kuzungumza naye, nami nikamwuliza, "Lilitukia saa ngapi?" ilikuwa ni saa ile ile tulipoenda kuomba.

Loo, Yeye … Yeye si ni wa ajabu! Ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Nina furaha sana kujua ya kwamba ninaishi katika Uwepo wa Mfalme.

140 Hebu na tuinamishe vichwa vyetu sasa, na ndugu mdogo wa thamani yuko hapa, ndugu mmishenari, rafiki yangu, mshiriki wa Assemblies of God, ndugu mdogo wa thamani hapa. Ninamwita, "Creechy." Yeye alinena mambo mazuri sana. Ndugu Creech, ninakuita hivyo. Sijui niseme nini, wewe ni ndugu yangu na mtumishi mwenzangu katika mateso ya Yesu Kristo katika siku hii ya mwisho. Mungu na awabariki. Nami nafikiri Ndugu Tony alisema ya kamba ulikuwa utaliruhusu kusanyiko liondoke wakati huu, tunapoviinamisha vichwa vyetu. Vema, njoo.

MESSAGE hub online

Mahubiri Na
William Marrion Branham
"... katika siku za sauti ..." Ufu. 10:7

www.messagehub.info